



BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE

AN AGENCY OF THE BAPTIST MISSION OF EAST AFRICA
TELEPHONE 58744 · P. O. BOX 30370 · NAIROBI, KENYA



IWE NURU



1. Isaac Lucy Kainage (Kiimel) Wambui.
2. Adje - Beatrix (Kiimel)
3. Jane Wani (Silome Muthuri).
4. Salula - Jane (Kike
Chintika)
- 5 -

IWE NURU

JULAI, AGOSTI, SEPTEMBER

1981

YALIYOMO

JULAI: HABARI ZA WABATISTI:

Mwandishi, Joan Carter

- 7 1. Asili ya Wabatisti
- 14 2. Wabatisti wa Kwanza
- 21 3. Wabatisti wa Liberia na Nigeria
- 28 4. Malawi, Zambia na Zimbabwe

AGOSTI: UKRISTO HUYALETA MABADILIKO:

Mwandishi, Pat Coursey

- 4 5. Mabadiliko Ndani ya Mtu
- 11 6. Mambo Yale Yamebadilika
- 18 7. Mabadiliko Kati ya Mtu na Mwenzake
- 25 8. Mambo Mapya ya Kweli

SEPTEMBER: FURAHA YA KWELI:

Mwandishi, Joan Carter

- 1 9. Furaha wakati wa Hitaji Letu Kuu
- 8 10. Furaha Katika Kuishi Maisha ya Kikristo
- 15 11. Furaha Katika Kuteswa kwa Ajili ya Yesu
- 22 12. Njaa Ulimwenguni *Plan Emergency Mission -*
- 29 - *Meet at my house -*

Misaada Maalum: Ugonjwa wa Kuhara

Mwandishi, Lynn Davis

© Copyright, 1981
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Likoni Road, Nairobi



CHUMVI



SUKARI

JULAI

Mpango wa Kwanza

ASILI YA WABATISTI

Kiini cha Mwezi: Habari za Wabatisti

Maandiko Matakatifu: 2 Timotheo 3:14-16

Kifungu cha Kukumbuka:

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu,"

Waefeso 2:8, 9

Utangulizi:

Je, kunaye mtu ye yote aliyepata kukuuliza kwamba ni nani aliyeanzisha kanisa la Kibatisti? Je, ulijua jinsi ya kumjibu? Pengine marafiki zake wamekwisha kumwambia kwamba imani ya Kibatisti ni kitu kigeni. Hii ni kweli? Tunahitaji kujua habari za Wabatisti, na tunahitaji kujua historia ya Wabatisti ili ndipo tupate kutoa majibu yaliyo kamili. Kwa muda wa majuma manne tutajifunza habari za Wabatisti ili ndipo tupate kujua mwanzo wao. Baadaye tutajifunza zaidi kuhusu Wabatisti na jinsi walivyoanza.

Je, habari za kanisa lako lilianza lini? Habari za kanisa lako zilianza kabla ya siku ambayo Wabatisti walianzisha kanisa katika kijiji chenu. Ilianza katika siku za Agano Jipya. Lakini ni kitu gani kilichotukia kati ya habari za Agano Jipya na kanisa lako la siku hizi? Muda wa miaka elfu mbili imekwisha malizika ikiwa na watu wengi pamoja na mambo mengi. Watu wengine walikuwa wazuri, wengine wabaya, wengine hodari na wengine waoga. Ebu na tutazame miaka thelathini baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni.

Sehemu ya Kwanza: Mekanisa ya Mwanzo (A.D. 100-600)

(Tazama: katika somo hili utaona ya kwamba herufi A.D. zimeandikwa zikitangulia tarakimu za mwaka. Katika lugha ya Kilatini Maana ya A.D. ni kusema "Anno Domino" yaani "miaka ya Bwana wetu." Hutumiwa kuonyesha kwamba mwaka huo ni kutoka wakati ambao Yesu alipozaliwa hapa duniani.) Wakati watu walipomwamini Yesu, waliunda mekanisa. Mekanisa hayo ya kwanza hayakuitwa "Baptisti" wala Katoliki au kwa jina lingine. Yalikuwa makundi ya mahali fulani ya Wakristo waliokutana pamoja, kuomba na kujifunza. Walishiriki na kushuhudia kama vile Yesu alivyowafundisha. Katika Rumi maadui wa Wakristo walimfanya Mfalme wa Kirumi kuwachukia Wakristo. Katika mwaka wa A.D. 64, moto mkali ulichoma sehemu zenye maskini katika mji huo wa Roma. Nao Wakristo walizingiziwa kuwa ni wao waliotekeleza mji huo. Nayo miaka na mateso mengi yalifuata.

Katika miaka hiyo Wakristo wengi waliuawa, na wengine waliangikwa msalabani. Warumi waliwamwagia Wakristo mafuta kisha wakawatekeleza moto wakiwa hali ya kufungwa mtini au kutupwa kwenye tundu la wanyama wakali, kama simba. Kwa muda wa miaka mia mbili na hamsini baada ya kifo chake Paulo, Wakristo walikuwa wakiabudu kwa siri. Kila mara walipata kutishwa kwa kifo.

Katika mwaka wa A.D. 323 Constantine alipata kuwa Mfalme wa Kirumi. Alitawala hata kila mtu alikuwa na uhuru wa kuabudu kama vile alivyotaka. Kwa mara ya kwanza, haikuwa kinyume cha sheria mtu kuwa Mkristo. Constantine alijaribu kuifanya dini ya Kikristo kuwa dini ya serikali yake. Hata alifikiria kwamba angaliweza kufanya askari wake wote kuwa Wakristo kama wote wangebatizwa.

Kutumia chupa kumlisha mtoto ni sababu kubwa kwa watoto kuhara. Kwa mama kumnyonyesha mtoto ni njia bora kumlisha mtoto. Kama mama hayuko na ni lazima kutumia njia nyingine kumlisha mtoto, tumia kijiko na kikombe. Usitumie chupa. Wenye duka watasema chupa ni njia ya kisasa kumlisha mtoto. Wanataka tu kuuza chupa. Kwa matajiri wenye jiko ya stima na maji ya moto ndani ya nyumba, labda ni njia nzuri. Kwa wananchi wote, kutumia matiti ya mama inafaa. Pia, kutumia kijiko na kikombe inafaa. Mdomo ya chupa ni mdogo. Huwezi kuweka mkono ndani kusafisha vizuri. Maziwa yatakaa ndani na vijidudu watakaa. Wataleta ugonjwa. Lakini wote wanavyo vikombe na vijiko, na wanaweza kuvisafisha vizuri.

Sababu nyingine ni uchafu kwa mikono ya watoto au ya mama. Ni njia ya maana sana kwa mama kunawa na sabuni kabla ya kutengeneza chakula au kabla ya kumlisha mtoto. Kama mtoto anaweza kujilisha, mfundishe jinsi ya kunawa vizuri. Tena baada ya kwenda choo ni saa ya kunawa ingawa si saa ya kula.

Kama mtoto anahara, mama anaweza kutengeneza dawa huko nyumbani kumsaidia. Dawa ni kikombe cha maji pamoja na sukari kama kipimo cha mkono mmoja na kiasi cha chumvi kama vidole vitatu. (Angalia picha). Mama atatengeneza hii mara tatu au mara nne kila siku kumpa mtoto. Atatumia kwa siku nne. Mama atakumbuka sababu ya kuleta ugonjwa huu na angalia. Mtoto akikosa kupona peke yake, mchukue kumwona daktari. Mara nyingi, atapona na dawa ya nyum' rni bila kumwona daktari. Kutumia dawa ya nyumbani bila kuangalia sababu ya kuhara ni bure. Dawa pamoja na bidii ya mama ni nzuri.

Tazama picha ukurasa wa 60.

mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Ebu na tuwahurumie wenye njaa kama vile Yesu alivyofanya. Ikiwa kuna njaa katika nchi yenu, jitayarisheni kuwasaidia wengine. Unapotoa sadaka yako katika Siku ya Maombi katika mwezi wa Novemba, sehemu yake nyingine itawasaidia watu walio na njaa.

Wewe uliye mke mwema, jaribu kuona ya kwamba jamaa zako wana chakula cha kutosha. Hakikisha kwamba wamepata chakula kinacholeta afya katika miili yao. Jifunze kulima sawasawa ili upate chakula kinachofaa kwa ajili ya jamaa yenu na kushirikisha wengine. Jifunze jinsi ya kuhifadhi chakula ili kisiharibike. Mwombe Mungu akusaidie kushiriki na wengine walio na njaa.

Maombi

MISAADA MAALUM

Ugonjwa wa Kuhara

Ni kama kawaida kwa watoto kuhara na kutapika mara kwa mara. Mara nyingine wanapona wenyewe. Pengine wanashida sana. Pengine wanakufa. Kwa nini?

Sababu ni nyingi.

Sababu moja ni maji. Ni vizuri sana kumpa mtoto maji ya kunywa. Lakini kwa watoto ni lazima kuchemsha maji kwanza kuwaua vijidudu wadogo ambao wataleta ugonjwa. Unafikiri kwamba watu wakubwa wanaweza kunywa maji bila kuyachemsha? Ni kweli; lakini watu wakubwa wanayo nguvu ya kuzuia ugonjwa kuliko watoto.

Sehemu ya Pili: Makanisa Baada ya Kuanguka kwa Rumi (A.D. 600-1517)

Kwa muda wa miaka mia sita utawala wa Kirumi ulikua na ukaenea katika sehemu zote ambazo siku hizi tunaziita Yoropa. Kila mahali Warumi walipokwenda, walipeleka dini ya Kristo na waliyalinda makanisa. Halafu ufalme wa Kirumi ulianguka. Kwa muda wa miaka mia tano baada ya kuanguka kwa utawala wa Kirumi kulikuwa na wakati ulioitwa "Miaka ya Giza". Zamani hizo kulitokea kuwa Papa kwa mara ya kwanza. Kulikuwa na falme ndogondogo. Jeshi la Papa lilishinda katika vita vingi na likashinda majeshi ya wafalme na watawala wengi. Chini ya Papa kanisa lilipata kuwa na utajiri mwingi na lilipata nguvu nyingi na liliweza kutawala nchi nyingi. Wakristo wachache ambao hawakukubaliana naye walipaswa kujificha ili waepuke mateso au kifo.

Watu wengi wapotea mbali hawakujua vile Biblia ilivyofundisha. Hawakuisoma Biblia ili ndipo wajue imani yao. Kwa mfano, waliamini kwamba mtu anapaswa kubatizwa ili ndipo awe Mkristo. Kwa sababu watu wengi hawakuweza kujisomea wao wenyewe, walijua tu kufanya yale yaliyoambiwa kufanya. Walihudhuria kanisani. Walibatizwa. Waliyafanya mambo mengine ambayo makasisi waliwaambia kufanya. Lakini hawakubadilisha njia zao za maisha. Kila kitu kilichofanywa katika ibada kiliendeshwa kwa lugha ya Kilatini, lakini watu hawakuongea wala kusikia Kilatini. Kwa hiyo, hawakufahamu yale yaliyosemwa. Hata wakati huo, Wakristo wengi wa kweli walikuwa wakifuata njia zake Kristo.

Sehemu ya Tatu: Martin Luther (1517-1600 A.D.)

Watu wengine walianza kujifikiria. Hata wengine walianza kuwa na maswali juu ya kanisa. Wakati huo ulijulikana kama wakati wa matengenezo, wakati ambao Wakristo walijaribu kuondoa shida ndani ya kanisa.

Kasisi mmoja aliyeitwa Martin Luther alileta shida kubwa kanisani katika mwaka wa 1517. Aliandika orodha ya visa tisini na tano kuhusu kanisa ambavyo alifikiria kwamba vinahitaji kuzungumzwa habari zake. Aliandika orodha hii na akaibandika juu ya lango la chuqikuu wakati wa sherehe. Jambo hilo lilileta makelele mengi. Hakutaka kuacha kanisa la Rumi. Alitaka tu kutengeneza mambo yaliyokuwa mabaya, lakini Papa hakukubali mabadiliko. Kwa hiyo Luther alianzisha kanisa la Kilutheri (Lutheran Church).

Viongozi wengine wa dini pia walikataa imani zingine na matendo ya desturi za kanisa. Nao walilazimishwa kuondoka kanisani. Nao watu hao walianzisha makanisa mengine yale tunayoyajua siku hizi kama Anglikana na Makanisa ya Kipresbyteria. Kila moja la makanisa hayo lilisaidiwa na serikali ya nchi ile lilipoanzishwa.

Sehemu ya Nne: Mitambo ya Uchapaji

Katika mwaka 1500 mashine za uchapaji zilikuwa zimekwisha gunduliwa. Kabla ya wakati huo vitabu vyote vilikuwa vikinakiliwa kwa mikono. Baada ya watu kuwa na ujuzi wa kuandika vitabu, Biblia pamoja na vitabu vingine viliweza kuandikwa kwa wingi. Watu walianza kujifunza kusoma. Waliweza kufasiri Biblia katika lugha zingine bila kutegemea lugha ya Kilatini peke yake. Watu walisoma Biblia na walijifunza ya kwamba mafundisho mengi ya kanisa Kirumi hayakulingana na Biblia.

Sehemu ya Tano: Anabaptists na Wengine

Vikundi vingine vingi vilianza kukutana vikijaribu kuabudu kama vile Biblia inavyoeleza. Baadhi ya vikundi hivyo viliitwa Lolards, Anabaptists, na Mennonites. Vikundi hivyo vinafanana na Wabatisti. Watu wa makundi hayo waliteswa na wengine waliuawa kwa sababu walikataa kufuata dini ya Serikali katika nchi zao.

Sehemu ya Nne: Chakula Zaidi, Chakula Bora

Tumekwishaona njia zingine nyingi ambazo Wabatisti husaidia kutoa chakula wakati wa hali ya hatari ya njaa. Kunazo njia zingine za kusaidia kumaliza njaa pia. Wabatisti huwasaidia watu kuwa na chakula bora katika sehemu nyingi.

Mmisheni wa kufanya kazi ya kufundisha ukulima anaishi katika nchi ya Botswana. Yeye huwasaidia watu wa nchi hiyo kavu kujifunza njia bora za ukulima ili waweze kupata chakula zaidi.

Wakati wa vita katika nchi ya Uganda wakati ule Amini alipopinduliwa, chakula kingi kiliharibiwa na majeshi. Watu wengi waliacha nyumba zao na hawakuweza kupanda tena. Baadaye Wabatisti walisaidia kwa njia ya kugawa vyombo vya kulimia ili kuwasaidia watu kupanda tena, pamoja na kugawa chakula na dawa.

Katika nchi ya Zimbabwe Mmisheni mmoja daktari aliwafundisha watu jinsi ya kufuga sungura. Watu wanaweza kula sungura. Watoto wanaweza kupata nyama ili afya yao iwe bora.

Katika nchi ya Bangladesh, inayopakana na nchi ya India, mmisheni wa Kibatisti aliwasaidia watu kuwa na vidimbwi vya kuwafuga samaki. Wao huchimba vidimbwi vya maji kisha wanawaweka samaki. Nao samaki huanza kuzaana upesi sana. Halafu watu huanza kuzila. Samaki huwa ni chakula kizuri kwa afya.

Hizi ndizo njia zingine ambazo Wabatisti husaidia katika kuzuia njaa.

Kiongozi:

Je, ungependa kumpikia Yesu chakula? Je, ungependa kumshirikisha chakula chako? Yesu alisema, "Kadri

ambao wazazi wao waliuawa na mashifta. Mashifta ni watu wale wanaotoka nchi ya Somalia kuja kudai sehemu za nchi ya Kenya kuwa yao. Watu wale waliofika kutoa chakula walikuwa wakishuhudia habari za Yesu safarini mwao.

Kunazo sehemu nyingi katika nchi ya Afrika ambako msaada wa aina hii umefanywa.

Sehemu ya Tatu: Dhoruba na Tetemeko la Nchi

Upepo mkali ulivuma katika kiziwa cha Dominika katika mwaka wa 1979. Nchi hii ndogo haiko mbali kutoka Amerika. Wakati upepo ulipokoma kuvuma, watu elfu kumi na tano walikuwa wamekwisha fariki. Nyumba za watu wapatao elfu mia mbili ziliharibiwa. Upepo ulikuwa umekwisha kuharibu mimea na miti ya matunda. Upepo ulichukua maji kutoka baharini na yakaingia katika nyumba za watu. Karibu kila kitu kiliharibiwa na upepo huo au mafuriko hayo. Hakukuwa na chakula!

Wabatisti walikuwa baadhi ya watu wale waliotuma msaada. Walituma ndege zenye kubeba furushi za mchele na maharagwe. Walipeleka madawa. Waliwatuma watu kwenda kugawa chakula na dawa na kujenga makao ya muda. Daraja zilichukuliwa na maji kwa hiyo watu wengi waliokuwa vijijini hawakuweza kutoka. Wabatisti walipeleka chakula kwa watu wa vijiji fulani ambako watu hawakupata chakula kwa muda wa siku nne.

Katika mwaka wa 1980 tetemeko la nchi lilitukia katika nchi ya Italia. Nyumba za watu elfu nyingi ziliharibiwa. Ulikuwa wakati wenye majira yenye baridi. Wabatisti walikuwa watu wa kwanza kufika kuwaletaka chakula cha moto kwa hao watu.

Mwisho:

Wakristo wanaompenda Yesu wanapenda kufuata mafundisho ya Biblia. Mara nyingi katika historia watu waliacha njia ya mafundisho haya. Ebu na tuhakikishe kwamba tumejifunza Neno Lake ili tuweze kuzifuata nyayo zake Yesu. Ebu na tuyasaidie makanisa yetu kuwa kama makanisa ya Agano Jipya.

JULAI

Mpango wa Pili

WABATISTI WA KWANZA**Kiini cha Mwezi:** Habari za Wabatisti**Maandiko Matakatiifu:** Matendo 4:18-22**Kifungu cha Kukumbuka:***"Petro na Mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu."**Matendo 5:29***Utangulizi:**

Mara kwa mara ikiwa mtu anataka kumtii Mungu, ni lazima avunje sheria. Ni lazima akate shauri kama anataka kumtii Mungu au mwanadamu.

Karibu muda wa miaka mia nne iliyopita katika mwaka wa 1600 katika nchi ya Uingereza, kulikuwa na kanisa moja tu lililotambuliwa na serikali. Mfalme ndiye aliyekuwa kichwa cha kanisa. Ikiwa watu hawakuwa watii kwa kanisa hilo mfalme alifikiria kwamba siyo waaminifu kwake.

Kanisa lilikuwa likisaidiwa na serikali. Watu walilipa kodi kwa kulitegemeza kanisa.

Wakati Biblia ilipochapishwa kule Uingereza katika Karne ya 16 kwa lugha ya watu hao, wale walioisoma au kuichapa waliteswa hata waliuawa. Katika mwaka wa 1600, Biblia katika lugha ya Kingereza ilikubaliwa. Lakini watu walipoanza kuisoma Biblia, walianza kuwa na mashaka kuhusu mambo yale yaliyokuwa yakitendwa na kanisa. Watu wengine walianza kukutana mahali pengine, nao wakaanza kuitwa "non-conformists" yaani wale wasiyofungwa na desturi za kanisa. Walikuwa wavunja sheria.

yao. Pia hali ya anga haikuwa nzuri. Kwa sababu ya vita, mateso na majira mabaya kuendelea, watu hawakuweza kupanda vyakula. Hapakuwa na mavuno kwa muda wa miaka minne. Maisha yalibadilika kuwa mabaya sana mpaka watu hao wakalazimishwa kuacha nchi yao. Walihama wakaingia katika nchi ya Thailand. Na wengine wengi wangali wakiendelea kuingia.

Serikali ya Thailand imeanza kujenga kambi za wakimbiaji. Wabatisti husaidia katika kambi hizo. Wamewatuma madaktari wa kuwatibu wagonjwa. Hugawa chakula kile kilichotumwa kutoka katika nchi zingine.

Mtu mmoja alisema, "Watu hawa hufanya kama kwamba wamesahau njia ya kula". Wengi wao huwa karibu kufa wanapowasili. Mara kwa mara watoto huja peke yao. Wametenganishwa na wazazi wao katika safari yao ndefu au wazazi wao wamekwisha kufa.

Wabatisti hujaribu kuwalisha watoto wachanga na akina mama wanaonyonyesha kwanza. Wanajaribu kufanya jamaa wapate wenzao tena.

Pia Wabatisti hutoa habari za Yesu. Mmisheni mmoja peke yake amekwisha kuwabatiza zaidi ya wakimbizi 2,000 tangu walipoanza kufika.

Sehemu
Sehemu ya Pili: Ukame Katika Bara la Afrika

Nyakati zingine mvua hufika kama imechelewa. Wakati mwingine mvua inakosa kufika. Jambo hili likitukia mahali popote katika Afrika, mara hutokea njaa.

Katika Mkoa wa kaskazini magharibi mwa Kenya mapema mwaka wa 1981, kulikuwa na watu wengi wenye njaa. Chakula kilitumwa kutoka katika sehemu nyingi za mataifa ya ulimwengu. Baadhi ya watu hao walikuwako watoto wale

SEPTEMBER

Mpango wa Nne

NJAA ULIMWENGUNI**Maandiko Matakifu: Mathayo 25:34-40****Kifungu cha Kukumbuka:***"Amini, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"**Mathayo 25:40***Kiongozi wa Mpango:**

Je, siku moja umewahi kuwa na njaa, njaa kali kabisa? Je, unakumbuka jinsi ulivyochoka? Unakumbuka jinsi ulivyokuwa na wasiwasi kuhusu chakula cha watoto wako? Je, uliogopa kwamba wewe mwenyewe utakufa?

Yesu alifahamu kuhusu mambo ya njaa. Alipokuwa hapa duniani aliwalisha watu elfu nyingi waliokuwa na njaa. Pia aliwafundisha wafuasi wake kuwahurumia wenye njaa. Alisema, "Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Kunao watu wengi duniani siku hizi wenye njaa. Wengine wamepata njaa kwa sababu ya vita. Wengine wamepata njaa kwa sababu ya tetemeko la ardhi au kwa ajili ya dhoruba. Wengine wamepata kwa sababu ya ukosefu wa mvua au kwa sababu ya kuwa na mvua nyingi. Leo tutajifunza vile Wabatisti huwasaidia baadhi ya watu hao wenye njaa. Huwapa chakula. Pia huwajulisha habari za Yesu, ambaye ndiye Mkate wa Uzima.

Sehemu ya Kwanza: Wakimbizi Katika Nchi ya Cambodia

Nchi ya Cambodia (Kampuchea) iko mbali sana. Iko karibu na Uchina. Kwa muda wa miaka mingi kulikuwa na vita vingi katika nchi hiyo. Watu wa nchi hiyo wameteswa sana na serikali

Je, kulitukia nini wakati watu hao walipoanza kuabudu katika sehemu zingine badala ya kuingia katika kanisa la Kianglikana? Kulitukia nini walipoanza kufanya mambo kwa njia tofauti? Mpango wetu wa leo utatueleza juu ya watu fulani ambao walitii kufuata mafundisho ya Mungu kama vile walivyoyafahamu toka katika Biblia.

Sehemu ya Kwanza: Wabatisti wa Kwanza

Katika mwaka wa 1600 mtu aitwaye Thomas Helwys na kundi la Wakristo wengine katika Uingereza walikutana kwa siri kujifunza Neno la Mungu. Walitaka kuwa raia waaminifu, lakini pia walitaka kumtii Mungu. Walifahamu kwamba Biblia ilifundisha kuwa ni watu wale wanaomwamini Yesu wanaopaswa kubatizwa. Lakini kanisa la Kianglikana linasema *kwamba* ni lazima watoto wachanga wabatizwe.

Walikataa kuwabatiza watoto wachanga. Kwa sababu ya jambo hili walidhulumiwa kupewa faini kali. Nao wengine walifungwa gereza.

Mwishowe watu wanane kati yao, waume, wanawake na watoto wao, walikimbilia nchi ya Uholanzi kuepuka kufungwa gereza. Walipowasili kule, waliwabatiza watu wazima wote waliomwamini Yesu. Kule katika nchi ya Uholanzi walikuwa wakikutana katika nyumba za watu. Baadaye walikata shauri kurudi katika Uingezeza kupeleka ukweli ule ambao walikuwa wamekwisha kuupata.

Katika mwaka wa 1612 Thomas Helwys aliongoza kundi la watu kurudi mpaka Uingereza. Hata ikiwa walifahamu kwamba watateswa, walilianzisha kanisa. Naye Thomas Helwys kuchapa vijitabu vya kueleza imani yao. Hata alituma kijitabu kimoja kwake mfalme. Kwa sababu ya kufanya hivyo alitupwa gereza na alifariki kule gereza. Lakini watu wengi walikuwa wamekwisha kumwamini kwa sababu ya kuvisoma vijitabu

vyake. Nayo makundi mengine yalianza kukutana. Nayo makanisa mengine mengi yalianzishwa. Ingawa yalikuwa sawa na makanisa ya Kibatisti ya siku hizi, hayakuitwa makanisa ya Kibatisti mpaka mwaka wa 1650.

Miaka mingine baadaye, Uingereza ilikubali makanisa mengine kukutana na kumwabudu Mungu kama vile walivyopenda. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi.

Sehemu ya Pili: Wabatisti Katika Nchi ya Amerika

Baadhi ya kundi la kwanza la watu wale walioondoka Uingereza kwenda kuutafuta uhuru katika Amerika na kumwabudu Mungu kama vile walivyopenda walikuwa Wabatisti. Watu wengine walikwenda mpaka Amerika kumwabudu Mungu kama vile walivyopenda. Wakati mwingine watu hao hao hawakukubali kuwapa watu wengine uhuru kama huo. Kwa hiyo Wabatisti, pamoja na watu wengine, waliteswa.

Mmoja wa wale walioteswa kwa sababu ya dini alikuwa Roger Williams. Alilazimika kuondoka mji wa London kwa sababu ya imani yake. Alifika Amerika. Tena alikataa kuikana imani yake ya Kibatisti. Kwa hiyo alilazimishwa kuondoka mji wa Plymouth. Zamani zile karibu sehemu zote za nchi ya Amerika zilikuwa mbuga. Naye Roger Williams aliwajua Wahindi Wekundu, wazalendo wa kwanza wa nchi ya Amerika. Alijua lugha yao kwa sababu alikuwa amekwisha kwenda huko mapema kuhubiri. Walikuwa marafiki zake, kwa hiyo aliishi nao huko mbugani. Baadaye alianzisha makao mengine mapya ambako watu waliishi na kumwabudu Mungu kama vile wanavyopenda. Mahali hapo paliitwa Rhode Island. Kanisa la kwanza la Kibatisti katika nchi ya Amerika lilianza kule katika mwaka wa 1639.

Wakati nchi ya Amerika ilipojitawala, katiba ya nchi hiyo ilisema kwamba ni lazima kuwe na uhuru wa dini.

Mateso ni furaha kwa sababu Mkristo hushiriki katika mateso yake Yesu. "Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe" (1 Petro 4: 13). Paulo alisema kwamba alikuwa na furaha katika kuteswa. "Tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake" (Wakolosai 1:24). Yesu aliteswa ili kwa jina lake tupate uzima. Itachukua maisha ya Wakristo wengi kuleta ujumbe huo kwa ulimwenguni mwote.

Mwishowe Mkristo anayeteseka atashiriki katika furaha yake Kristo milele. Hii ndiyo sababu ya kumfanya afurahil

Mwisho:

Mafundisho ya Yesu kutoka katika Mathayo 5:1-12 ni kwa ajili ya Wakristo. Watu ambao bado hawajaamini hawawezi kuamini mambo hayo.

Pengine Wakristo wengine hawana furaha hii katika maisha yao. Anza mahali ulipol Yesu alisema, "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu" (Yohana 7:17). Mungu atatusaidia kufahamu ikiwa kwa kweli tunataka kuyajua mapenzi yake.

Wamekwisha kuwatesa Wakristo wanaoonyesha upendo badala ya chuki.

Sehemu ya Nne: Je, Mkristo Anapaswa Kufanya Nini?

Soma 2 Petro 3:12-18.

Mkristo anazo silaha mbili za kutumia wakati wa mateso. Silaha moja ni hiyo ya kuwa na *maisha safi*. Ni lazima Mkristo awe raia mwema na mtumishi mwema. Maisha yake yanapaswa kuwa mazuri hata wale wanaomsingizia wawe na aibu.

Silaha nyingine ni jibu la Mkristo, ushuhuda wa Mkristo. Ni lazima Mkristo ajue mafundisho ya Yesu ili apate kuwa tayari kutoa jibu lililo sawa. "Mwe tayari sikuzote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu" (1 Petro 3:15).

Sehemu ya Tano: Kwa Nini Mateso ni Furaha?

Mara kwa mara watu hawateswi ikiwa hawafaulu katika ushuhuda wao. Magaidi wengine katika nchi moja ya Kiafrika walithibitisha kwamba Wakristo hawawezi kujiunga nao katika kuwaua watu wengine. Waliona kwamba Wakristo walikuwa na mvuto kwa watu wengine na waliwazuia wasijiunge na magaidi hao. Magaidi waliwatesa Wakristo na kuwaua wengine ili kuzuia mvuto wao usiendelee. Watu wale walioteswa walikuwa na furaha kujua kwamba walifaulu.

Mateso ni furaha kwa sababu humpa Mkristo nafasi ya kuonyesha uaminifu wake. Anaweza kuthibitisha kwamba haionei haya injili yake Kristo.

Ni furaha kwa Mkristo kujua ya kuwa anafuata hatua za watakatifu, "Kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu" (Mathayo 5:11).

R. R. R.

Sehemu ya Tatu: Wabatisti na Uenezaji wa Injili

Kwa muda wa miaka mingi Wabatisti wa nchi ya Amerika na Uingereza walikuwa wakiihubiri injili kwa watu wa nchi zao peke yake. Lakini hawakuanza kuwatuma wamisheni mpaka mwaka wa 1792.

Mtu mmoja aliyeitwa William Carey alikuwa akiishi Uingereza. Alikuwa Mbatisti. Alikuwa mshona viatu, lakini alipenda kujifunza Biblia pamoja na ramani ya ulimwengu. Aliwahurumia sana watu wa ulimwengu ambao walikuwa hawajamjua Yesu Kristo bado. Alijisikia kwamba Mungu alikuwa akimwita kwenda mpaka nchi ya India kuhubiri, lakini hakuwa na pesa za kulipia nauli. Alizungumza na kundi la wahubiri Wabatisti kuhusu vile injili ilihitaji kuenezwa kwa watu waliopotea. Mzee mmoja alimwambia, "Kijana, keti chini. Mungu akipenda kuwaokoa watu wasiyo na dini, atafanya hivyo bila msaada wako wala wangu." Lakini watu wote hawakukubaliana naye. Walikata shauri kuunda chama cha kumtuma William Carey kama mmisheni. Alifika katika nchi ya India katika mwaka wa 1792. Hatimaye vyama vingine vya kuwatuma wamisheni viliundwa. Wamisheni wengine wengi walitumwa katika nchi ya India, hata na katika nchi za Burma na Uchina. Carey aliishi katika nchi ya India kwa muda wa miaka mingi akifasiri Biblia, kuhubiri na kuwabatiza wale waliookoka. Hakurudi tena katika nchi ya Uingereza, lakini alifariki akiwa kule India baada ya kuishi huko kwa muda wa miaka mingi.

Sehemu ya Nne: Southern Baptist Convention

Wabatisti wa Amerika walianza kuwatuma wamisheni katika mwaka wa 1814 wakati ambao waliunda jumuiya yao. Wamisheni wao wa kwanza walitumwa katika nchi ya Burma. Katika mwaka wa 1845, kulikuwa na kutopatana kwingi kati ya Wabatisti wa Amerika kuhusu kazi ya umisheni na vile watafanya kuhusu utumwa. Kwa sababu ya jambo hili,

Wabatisti walikata shauri kuunda Jumuiya ya Wabatisti iitwayo Southern Baptist Convention na nyingine iitwayo Northern Baptist Convention. (Sasa Northern Baptists wanaitwa American Baptists). Wabatisti wameendelea kukua katika nchi ya Amerika. Sasa kuna Wabatisti zaidi ya milioni 28. Kunazo Jumuiya saba za Wabatisti ambazo huwatumia wamisheni kwa kadiri ya nchi sabini.

Mwisho:

Wabatisti wamejulikana kama "watu wa Biblia." Ni watu ambao huiamini Biblia na wanapenda makanisa yao kuwa kama makanisa ya Agano Jipya. Zamani wengi wao walipata mateso mengi kwa sababu ya imani yao. Ebu na tuhakikishe kuhusu mafundisho ya Biblia ili tuweze kusimama imara katika yale tunayoyaamini. Wabatisti ni watu wanaojulikana kama watu wanaoamini katika uhuru wa kuabudu. Ebu na tuwe wavumilivu na wenye upendo kwa watu wale ambao hawaamini kama sisi.

hiyo walitaka kuwamaliza Wakristo kutoka katika ulimwengu huu. Halafu ndipo waendeleo katika dhambi zao.

Sehemu ya Tatu: Kwa Nini Wakristo Wanateswa Siku Hizi?

Siku hizi Wakristo wanateswa kwa sababu zile zile tu za zamani za Biblia.

Wanawake fulani wa kabila la Kimaasai katika nchi ya Kenya walimwamini Yesu. Waume zao hawakuwa Wakristo. Wanawake walipigwa na waume zao kwa sababu walikataa kushiriki katika desturi zao za kale zilizo mbovu. Desturi hizo ni kinyume cha mafundisho ya Biblia. Wamaasai ambao hawakuwa Wakristo walisema, "Wanavunja desturi zetu."

Wakristo wengi katika nchi wa Uganda walifariki, na wengine waliteswa sana chini ya utawala wa Amin. Walichagua kuteswa kuliko kumkana Yesu Kristo. Maisha yao mazuri yalimkemea Amin na watu wake.

Mwanamke Mkristo aliteswa kila wakati mume wake alipolewa pombe. Alimwaga maji sakafuni mwa nyumba yao na kumlazimisha mkewe kulalia maji. Kwa nini? Kila wakati alipomtazama na kuona jinsi alivyokuwa *mzuri*, alianza kukumbuka vile alivyokuwa *mbaya*. Jambo hili lilimfanya kukasirika *sana* mpaka akaanza kumwadhibu.

Vijana wengi Wakristo wamedhulumiwa na wenzao kwa sababu ya kukataa kunywa pombe au kutumia madawa. Wanateswa kwa sababu wao ni tofauti na wengine.

Wakristo wengine katika nchi ya Afrika wameteswa kwa sababu wamekataa kuwachukia watu wa mataifa mengine ambao wanaishi kati yao. Kwa sababu pendo la Yesu limo mioyoni mwao, walikataa kuwa na chuki au kuua wale wanaowatawala. Jamaa au marafiki zao na viongozi wa kabila lao wanaweza kuwafikiria Wakristo kama hawa kuwa wasaliti.

Sababu kubwa iliyofanya Wakristo kuteswa ni kwamba walikataa kumwabudu Kaisari kama Mungu. Kaisari alikuwa kiongozi wa ufalme wa Kiyahudi. Alikuwa akitawala nchi nyingi. Kila mtu alilazimika kusema, "Kaisari ndiye Bwana!" Sheria ililazimisha jambo hili. Wayahudi peke yake ndio waliokubaliwa wasifanye hivyo. Ikiwa mtu alikataa kusema, "Kaisari ni Bwana," watu na serikali walisema, "Yeye ni haini." Walisema kwamba "Yeye ni adui wa taifa." Serikali iliweza kumshika na kumwadhibu.

Sehemu ya Pili: Je, Waliteswa Kwa Njia Ipi?

Kwa maana walimwamini Yesu, maisha ya Wakristo yalikuwa tofauti kutoka kwa watu waliowazunguka. Wema wao uliyafanya maisha ya watu wale waliowazunguka kuonekana mabaya zaidi. Kwa hiyo watu wale wengine hawakuwapenda. Watu walinena maovu juu yao na waliwatusi. (Tazama 1 Petro 2:12).

Wakati mwingine waliharibu mali za Wakristo. "...tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo" (Waebrania 10:34).

Wakristo wengi waliteswa na kuuawa. Walitupwa kwa simba wakaliwa. Waliangikwa msalabani. Walichomwa moto wakafa au kutupwa baharini.

Walikataa kumwabudu Kaisari, jambo ambalo liliwafanya viongozi wa taifa kufikiria kwamba walikuwa wahaini. Walivunja desturi za watu hao. Walijitenga na matendo maovu ya watu wa zamani hizo. Wema wao kwa hali ya kimya ulikemea dhambi za watu wale waliowazunguka. Watu hawataki kuonyeshwa matendo maovu yaliyomo katika maisha yao. Kwa mumewe alikuwa akimwadhibu. Mara kwa mara alikuwa akimpa talaka.

JULAI

Mpango wa Tatu

WABATISTI WA LIBERIA NA NIGERIA

Kiini cha Mwezi: Habari za Wabatisti

Maandiko Matakatiifu: Warumi 10:8-13

Kifungu cha Kukumbuka:

"Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa?"

Warumi 10:14, 15a

Kiongozi wa Mpango:

Wiki iliyopita tulijifunza mambo fulani kuhusu historia ya Wabatisti na mianzo yao katika Ulaya na Amerika. Tulijifunza kwamba shirika za kueneza injili zilianzishwa kwa kusudi la kuwatuma wahubiri kwenda nchi zingine. Siku ya leo tutajifunza habari za Wabatisti wa kwanza katika Afrika. Wabatisti hawa walikuwa katika nchi za Liberia na Nigeria.

Sehemu ya Kwanza: Uhuru Katika Liberia

Katika mwaka wa 1700 Waafrika wengi walichukuliwa na kupelekwa Amerika wakiwa watumwa. Baadaye, watu wengine waliowanunua watumwa hao walianza kuona utumwa ni kitu kiovu kwa hivyo waliwaachilia huru watumwa wao. Katika mwaka wa 1820 kikundi cha watumwa hawa waliingia melini na kurudi Afrika kuanzisha serikali yao wenyewe. Halikuwa jambo rahisi kwa sababu watumwa hawa ambao sasa walikuwa huru walikuwa wamezaliwa Amerika. Hawakujua kabila lao wala mahali ambako babu zao walitoka. Hawakujua lugha yo yote ya Kiafrika, ila Kiingereza tu.

Kati ya watumwa hao waliokata shauri kurudi Afrika kulikuwamo na wahubiri wawili wa Kibatisti: Colin Teague na

Lott Carey. Wote wawili walijua kusoma. Carey alikuwa na elimu nzuri zaidi kuliko hao wote waliorudi. Alikuwa na shamba lake katika Amerika. Nauli yao ya wahubiri ya meli ya kuwapeleka Afrika ililipwa na Jumuiya ya "Triennial Convention" ili wafikapo wahubiri na kueneza injili. Kabla ya kuondoka, Wabatisti saba katika kikundi hicho walikutana na kuanzisha kanisa. Kwa hiyo, kanisa la kwanza la Kibatisti la Liberia lilianzishwa mwaka wa 1820 hata kabla ya watumwa hao kuwasili humo nchini.

Kikundi hiki kilikuja na kukaa katika nchi hii ambayo inajulikana kama Liberia. Wengi wao walitaka tu kujenga makao yao na kuishi kwa amani. Lakini iliwabidi kupigana vita kabla ya kuweza kukaa kwa amani. Waliyakuta makabila yaliyokuwa yakikaa humo ambayo walijaribu kupigana nao vita ili kuwafukuza. Tena wafanyi biashara ya utumwa walifika kwa njia ya meli na kujaribu kuwashika na kuwafanya kuwa watumwa tena. Katika mwaka wa 1847 baada ya kufanya jitihada nyingi, taifa la Liberia lilizaliwa.

Sehemu ya Pili: Lott Carey na Wabatisti Wengine

Lott Carey sikuzote aliona kwamba wajibu wa kwanza ni kuhubiri injili ya Yesu Kristo. Kanisa waliloanzisha kabla ya kuondoka Amerika lilikuwa Providence Baptist Church la Monrovia ambalo liko mpaka sasa. Carey akawa kiongozi katika serikali ya Liberia. Alikuwa liwali (Governor) wa nchi hiyo kwa muda. Pia, alikuwa mhubiri, mwalimu, na mlinzi wa nchi yake. Alikufa mwaka wa 1828 alipokuwa akijaribu kuisaidia nchi yake kupambana na meli iliyokuja kuwachukua watu wake kuwa watumwa.

Wamisheni walitumwa na Triennial Convention na baadaye na Southern Baptist Convention mpaka mwaka wa 1875. Wengi wa wamisheni hawa walikuwa Waamerika weusi, wengine walikuwa weupe. Wengi wao walikufa baada ya miaka

hawana adabu nzuri. Tukiwakaribisha hawakuja kwa karamu zetu. Hujitenga na watu wengine. Hujificha na kukutana gizani."

Ikiwa mtumwa angeongoka na kuwa Mkristo, Wakristo wale wengine walimwita "Ndugu". Msichana mzuri kutoka katika ukoo usio wa utumwa wenye maendeleo ya Kikristo aliolewa na mtumwa aliyeongoka na kuwa Mkristo. Kwa Warumi jambo hilo halikuwa halali. Lilikuwa jambo la kustaajabisha kwa watu wengine. Wao walisema kwamba "Wakristo wanavunja desturi zetu."

Ilikuwa ni vigumu Wakristo kupata kazi nzuri. Kama mtu angekuwa mwashi, angalijenga hekalu la wapagani. Kama angefanya kazi kama mshonaji wa nguo, angaliwashonea nguo makuhani wa dini yao. Kama mtu angalifanya kazi kama mwalimu, angalifundisha hadithi za miungu yao ya uongo. Wakristo wengi hawakupata kazi ambazo zilikuwa nzuri kwao. Watu walianza kusema "Wakristo ni wavivul"

Sababu nyingine iliyofanya Wakristo wengine kuteswa ilikuwa, Wakristo wengi walikuwa wa kabila la Kiyahudi. Idadi kubwa ya Wayahudi haikuamini Yesu Kristo. Wakati mwingine wao ndio walioyaongoza mateso ya kuwatesa Wakristo.

Wakristo hawakuabudu sanamu. Watu wa mataifa walishindwa kufahamu vile mtu angaliweza kuabudu bila ya kutumia sanamu. Walisema kwamba "Wakristo hawamwabudu Mungu!"

Watu walianza kusema uongo kuhusu Wakristo. Waliposikia habari za Meza ya Bwana walisema, "Wakristo huwala watu na kunywa damu yao."

Ukristo ulifanya miji mingi kuvunjika. Jambo hili lilikuwa kweli. Ikiwa mwanamke angaliongoka bila mumewe kuongoka kuwa Mkristo, kulikuwa na shida nyingi. Mara kwa mara

SEPTEMBER

Mpango wa Tatu

FURAHA YA KUTESWA KWA AJILI YA YESU**Kiini cha Mwezi:** Furaha ya Kweli**Maandiko Matakatifu:** 1 Petro 4:13-16**Kifungu cha Kukumbuka:***"Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao."**Mathayo 5:10***Utangulizi:**

Je, wewe unapenda kuudhiwa? Hashal Hata wakati wa zamani za Yesu watu hawakupenda kuudhiwa. Lilikuwa jambo geni Yesu kusema kwamba mtu anaweza kufurahi akiteswa. Unawezaje kufurahi unapoteswa? Leo tutajifunza jinsi ya kuwa na furaha ya kweli katika kuteswa kwa ajili ya Yesu.

Sehemu ya Kwanza: Sababu ya Kuteswa Kwa Wanafunzi wa Yesu

Yesu alisema, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuata" (Mathayo 16:24). Hakuna njia nyepesi ya kumfuata Yesu. Katika maisha yake yote, Yesu alifahamu kwamba atateswa na kuuawa msalabani. Aliwaambia wafuasi wake kwamba ni lazima watarajie mateso.

Baada ya Yesu kurudi kwa Babaye, Wakristo waliteswa kwa sababu nyingi. Zamani hizo Warumi walikuwa wakitawala nchi ambako Wakristo walikuwa wanaishi. Wakristo walikuwa tofauti kutoka kwa watu wale wengine. Ikiwa Wakristo walihudhuria karamu za sikukuu, kwa kawaida watu walikuwa wakitoa sadaka kwa miungu wao. Halafu walikuwa wakila chakula kilichotolewa sanamu hizo. Wakristo walikataa kula chakula cha karamu hizo. Watu walianza kusema, "Wakristo

michache. Mmoja kati ya wamisheni hao waliojulikana sana alikuwa John Day, ambaye alifanya kazi miaka mingi akianzisha makanisa na shule. Katika mwaka wa 1840 kulikuwa na makanisa ishirini na manne na washiriki 1,200.

Makanisa pia yalikuwa na matatizo. Washiriki wote ishirini wa kanisa moja la Kibatisti waliuawa na kabila la Bassa hapo mapema.

Mnamo mwaka wa 1880, makundi ya Wabatisti weusi wa Amerika walichukua wajibu wa Misheni ya Liberia. Walishughulika zaidi na wazao wa watumwa wa Amerika waliokaa katika mwambao wa pwani. Katika mwaka wa 1960 Southern Baptists waliombwa na Waliberia kuja kuendeleza shule zao, na kuwahubiria makabila wanaokaa bara ambao si Wakristo.

Katika mwaka wa 1980, Jumuiya ya Wabatisti wa Liberia (Liberian Baptist Convention) ilitoa ripoti kwamba kuna Wabatisti 42,620 katika Liberia. Rais wa zamani wa Liberia, Mheshimiwa Tolbert ndiye aliyekuwa mwenye kiti wa chama cha Wabatisti wote ulimwenguni (Baptist World Alliance) kuanzia mwaka wa 1965 mpaka 1970.

Sehemu ya Tatu: Mwanzo wa Wabatisti wa Nigeria

Thomas J. Bowen ndiye aliyekuwa mmisheni Mbatisti wa kwanza katika Nigeria. Alitumwa huko na Southern Baptists mwaka wa 1849 wakati ambapo Livingstone alipokuwa katika Afrika ya Mashariki na Kusini. Mtu wa kwanza kuamini wakati Bowen alipohubiri alikuwa mwanamke aliyeitwa Oyindou. Mwanamke huyu alileta sanamu zake zote alizokuwa akiziabudu ili zichomwe, akaomba abatizwe. Bowen alifungua vituo viwili katika sehemu ya kabila la Yoruba kabla ya kurudi Amerika kwa ajili ya afya mbaya.

Kwa muda wa miaka hamsini ya kwanza, kulikuwa na vizuizi vingi sana kwa kazi ya misheni huko Nigeria. Wamisheni wengi walikaa kwa muda mfupi tu kama miaka mitatu au minne hivi na kuondoka. Wengine walipatwa na mauti baada ya kukaa muda mfupi; na wengine walilazimika kuondoka haraka kwa sababu ya afya mbaya. Nao wengine waliondoka kwa sababu ya kuvunjika moyo. Kwa sababu ya vita iliyokuwako Amerika, ni wamisheni wachache sana waliotumwa kwa muda wa miaka mingi.

Vita vya ukabila katika Nigeria pia vilikuwa mojawapo ya vizuizi kwa kazi ya misheni. Wakati mmoja iliwabidi wamisheni kukimbia, na vyombo vyao vyote walivyoviacha viliangamizwa.

Baada ya kutumikia kwa miaka kadha kulitokea hali ya kutopatana kati ya wamisheni na raia wa Nigeria waliokuwa viongozi wa Kibatisti. Kisha wakaanza kugawanyika katika kazi.

Katika mwaka wa 1900, baada ya miaka hamsini, kulikuwa na makanisa sita tu ya Kibatisti na washiriki 385. Hata hivyo, msingi wa kuanzisha kazi ya Bwana ulikuwa umekwisha kuwekwa, kwa hiyo kazi haikuwa na budi kuendelea.

Sehemu ya Nne: Kukua kwa Kazi ya Mungu Nigeria

Kwa muda wa miaka michache iliyofuatia, wamisheni wengine zaidi walikuja. Makanisa yaliongezeka. Shule za Jumapili zilianzishwa na kazi ya utabibu ukaimarishwa. Umoja wa Wanawake ulianzishwa. Kazi ilianzishwa kwa kuwahubiria wenye ukoma. Mikutano ilifanywa ya wamisheni na watenda kazi Waafrika. Katika mwaka wa 1914, Jumuiya ya Yoruba iliundwa. Majola Agbedi ambaye aliongoza kikundi kile kilichopingana na wamisheni alichaguliwa kuwa mwenye kiti. Umoja kati ya Wabatisti ulianza tena kuwako na kuimarika. Jumuiya hii baadaye ikawa na Wabatisti wote wa Nigeria.

Mwisho:

Mungu wetu anaweza kutusaidia kuwa wapole, wenye huruma na walio safi ndani ya mioyo yao. Anaweza kutufanya kuwa wapatanishi. Je, jambo hili laonekana kuwa gumu? Jiweke kwake Mungu. Yeye atakufanya kuwa vile anavyotaka wewe uwe. Utaona furaha katika kukua ukifanana naye.

Yesu alisema kwamba wapatanishi wanayo furaha ya kweli. Kunao watu wanaopenda amani lakini hawafanyi jambo lo lote la kuleta amani. Wapatanishi wa kweli huwa tayari kuingia kwenye shida ili amani ipatikane.

Kunaye mwanamke ambaye ni mshiriki wa kanisa la Kibatisti, mume wake anakunywa pombe sana. Mara nyingi mumewe huwa hamtendi yaliyo mema. Lakini mwanamke huyo mara kwa mara anamsamehe mumewe. Anamwonyesha upendo na heshima. Ameleta amani. Kwa sababu hii huyo mwanamke anayo furaha, naye mumewe humheshimu na kumpenda.

Siku hizi ugomvi, kupigana na vita vinazidi kuendelea bila kukoma. Watoto hugombana. Mume na mke hupigana. Jirani hugombana. Nayo makabila na mataifa hupigana vita.

Wapatanishi hujaribu kufanya kazi ya kuvunja viambaza ambavyo huwatenganisha watu. Halafu wanaleta uhusiano bora kati yao na Mungu na wenzao.

Wakati wa jitihada ya kuhubiri Injili, watu wengi walimwamini Yesu. Mwanamke mmoja aliyeamini alisema, "Katika jitihada hii nimekwisha kumwamini Yesu, na ameniwezesha kusamehe mtu yule aliyemwua baba yangu." Ikiwa mtu anao uhusiano bora na Yesu Kristo, anaweza kusamehe na kuleta upatanisho kati ya watu.

Wapatanishi wataitwa wana wa Mungu. Je, siku moja umekwisha kumtazama mtoto, kisha ukasema, "Yeye amefanana na babaye?" Wapatanishi wamefanana na Baba yao, yaani Mungu. Huwa wanawasamehe watu na wanaleta watu hao kuwa na uhusiano bora na Mungu na watu wengine.

Kazi iliendelea kukua na kuenea upande wa kaskazini na kwa makabila mengine. Redio na Uchapishaji vitabu vilisaidia sana katika maendeleo ya makanisa na uenezaji wa Neno. Waafrika walianza kuchukua wajibu mkuu kwa kazi ya Bwana.

Makanisa na Jumuiya yalitegemeza shule nyingi na uchapishaji. Katika mwaka wa 1960 waliwatuma wamisheni raia wa Nigeria kwenda kuhubiri katika nchi ya Sierra Leone.

Katika mwaka wa 1980 idadi ya washiriki walikuwa 147,371 katika makanisa ya Kibatisti ya Nigeria.

Sehemu ya Tano: Kuenea kwa Injili Katika Afrika ya Magharibi

Hatuna wakati wala nafasi sasa ya kusimulia historia ya Wabatisti katika kila nchi ya Afrika ya magharibi, ila tutataja kwa kifupi nchi ambazo Wabatisti wanafanya kazi ya Bwana.

Wamisheni kutoka nchi nyingi wamekwisha kufanya kazi katika nchi ya Cameroons. Kwanza ilitembelewa na Wabatisti wa Uingereza katika mwaka wa 1876. Halafu Wabatisti wa Ujerumani na Amerika walituma wafanya kazi.

Makanisa yalianzishwa katika Sierra Leone na wamisheni kutoka Liberia. Makanisa ya kwanza ya Kibatisti katika Ghana Togo, na Ivory Coast yalianzishwa na watu wa Nigeria.

Southern Baptist Convention ya Amerika pia walianzisha kazi miaka michache iliyopita katika Senegal na Dahomey ambako lugha inayotumiwa ni ya Kifaransa, na pia katika Upper Volta.

Kiongozi:

Kazi ya kueneza Injili imekuwa imezuiliwa na vita, vifo, na magonjwa. Imekuwa ikipingwa na ukosefu wa upendo na udhaifu wa wanadamu, lakini hata hivyo, Neno la Mungu limeenea. Tumshukuru Mungu kwa kazi yake ya ajabul

JULAI

Mpango wa Nne

MALAWI, ZAMBIA, NA ZIMBABWE**Kiini cha Mwezi:** Zaburi 67**Kifungu cha Kukumbuka:***"Njia yake ijulike duniani, wokovu wake katikati ya mataifa yote."**Zaburi 67:2***Utangulizi:**

Katika Zaburi 67 mwandishi aanza kwa kusema, "Mungu na utufadhili na kutubariki, na kutuangazia uso wake. Njia yake ijulikane duniani, wokovu wake katikati ya mataifa yote" (Zaburi 67:1, 2). Mungu amekuwa mfadhili kwa watu wa Zimbabwe, Zambia na Malawi. Katika nchi hizo kumekuwa na shida nyingi, lakini Mungu aliendelea tu kubariki na kuongeza idadi nyingi ya wanaokolewa. Je, Wabatisti waliuchukua wajibu gani katika kuwaletea baraka za Mungu? Leo tutafikiria habari za kazi za Wabatisti katika nchi hizi ili tuweze kujifunza vile wamekwisha fanya ili ndipo njia zake zijulikane.

Sehemu ya Kwanza: Wabatisti Katika Malawi

Mwanzo wa Wabatisti katika nchi ya Malawi (ambayo hapo mbeleni ilikuwa ikiitwa Nyasaland) ni tangu mwaka wa 1892. Wabatisti kutoka Australia walianzisha kazi ya ukulima na viwanda karibu na mji wa Blantyre. Mtu mmoja aliyekubali neno walipohubiri alikuwa ni John Chilembwe. Alikwenda Amerika kujifunza. Baadaye alirudi akiwa na fedha za msada alizopewa na marafiki huko Amerika. Chilembwe na baadhi ya wafuasi wake waliuawa alipojaribu kuipindua serikali ya Waingereza, lakini kazi yake iliendelea. Mwafrika mwingine aitwaye Dr. Daniel Malekebu alipata mafunzo yake Amerika. Alihitimu shahada ya udaktari. Alirudi na akaanzisha Providence

Sehemu ya Tatu: Furaha ya Kweli kwa Wenye Moyo Safi

"Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu" (Mathayo 5:8). Mavuno mengi ya nafaka katika bara Afrika, hayahifadhiwi kwa njia bora. Hayakaushwi vizuri kabla ya kuwekwa ghalani. Kwa hiyo mahindi hupata koga. Hiyo koga inaweza kukosa kuonekana. Nafaka huonekana kama nzuri, lakini siyo nzuri. Koga hiyo ni sumu kwa watu na wanyama. Wanyama wengi hufariki wakila nafaka hizo. Pia nafaka hizo zaweza kuleta kifo kwa wanadamu. Nje nafaka huonekana kama nzuri, lakini siyo safi. Huwa na kutu au koga ndani yake.

"Walio safi wa moyo" ndio wale walio safi. Wamesamehewa dhambi zao. Hawana mambo machafu yaliyo changanywa ndani ya mioyo yao.

Watu wa zamani zile za Yesu walifikiria kwamba usafi hupimwa kwa njia ya kufuata torati na kujitawadha. Yesu aliwaambia kwamba walikuwa wakiosha *nje* ya kikombe (Luka 11:39). Aliwashauri kusafisha ndani ya moyo; halafu mambo yote yataonekana safi! Siku hizi pia kuna watu "wanaojifanya kuwa safi nje." Wao huhudhuria kanisa siku ya Jumapili, hutoa sadaka na husoma Biblia. Ukiwaona nje unaweza kufikiria kwamba wao ni Wakristo. Lakini mawazo na nia zao ni mbovu. Mpaka moyo wa mtu huyo uwe safi, hatakuwa safi au kuwa mwenye furaha.

Dhawabu ya moyo safi ni kwamba watamwona Mungu. Mtu hatamwona Mungu ikiwa kuna dhambi ndani ya maisha yake. Wale ambao kati yao na Mwokozi amekuwa safi ndio wawezao kumwona Mungu.

Elizabeth
Sehemu ya Nne: Wenye Furaha ya Kweli Ndio Walio Wapatanishi

"Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu" (Mathayo 5:9).

alitaka kumwuza mtumwa wake pamoja na jamaa yake kuwa watumwa ili alipie deni lake. Wakati mtu huyo alipoomba msamaha, bwanaye alimsamehe. Mtumwa huyo alipoondoka alienda akamkuta mtumwa mwenzake aliyekuwa na deni lake ndogo. Alidai alipwe deni lake na aliposhindwa kulipa alimtupa gerezani. Mtumwa huyo hakuonyesha huruma kwa mtumwa mwenzake.

Kila mara Mungu ameonyesha huruma kwa watu wake. Tunaona hivyo alipowakomboa wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri, alipomwokoa Lutu kutoka Sodoma na alipoyahifadhi maisha ya Yusufu. Tunaokolewa kwa sababu ya rehema yake. "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyo yatenda sisi, bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu" (Tito 3:5).

Rehema haikujulikana katika ulimwengu wa kipagani. Watoto mapacha wakizaliwa hawakuonyeshwa huruma. Mapacha mmoja au wote wawili wangaliuawa. Iwapo mtu alikuwa kiwete au kipofu, watu walimcheka. Mtu akipata kutenda jambo mbaya lililo ovu, hangalisamehewa. Aliweza kuadhibiwa au kutoroka akiwa na aibu. Desturi za makabila mengi, msichana huwa alikatwa sehemu zote za mwili na kila mahali palikuwa na alama ya urembo. Hawakujali hata ikiwa sehemu zile zilizokatwa zimeambukizwa na kuvimba. Hakuna mtu aliyemhurumia. Mambo mengi ya hayo yangali yakiendelea hadi sasa.

Rehema ni upendo katika matendo. Ni upendo ambao haupatikani katika torati. Moyo wa huruma kumfanya Mkristo kuona na kufahamu mateso ya wale ambao watu wengine hawawajali. Huruma humfanya Mkristo kufahamu shida za mtu mwingine kisha humsamehe.

Wale wanaoonyesha huruma watapokea huruma ya Mungu. Mungu hufahamu, husamehe na huokoa.

Industrial Mission. National Baptist Convention (ambayo ilikuwa Jumuiya ya Waamerika weusi) ilimsaidia sana kwa kazi yake, na baada ya muda si muda, wakawa na hospitali, shule, na makanisa katika Malawi, Zambia na Zimbabwe.

Southern Baptist Convention ya Amerika ilianza kuwatuma wamisheni Malawi katika mwaka wa 1959. Mwaka ule William na Blanche Wester waliondoka Zimbabwe kwenda Blantyre pamoja na Roy na Jean Albright. Wao waliifungua kazi kule Lilongwe. Naye Kingsley na jamaa yake walijiunga na wamisheni wa Malawi katika mwaka wa 1960. Katika mwaka wa 1964 Malawi ilipata uhuru wake chini ya uongozi wa Dr. Hasting Banda. Shule ya Biblia ya kuwafundisha wachungaji na jumba la Uchapishaji vitabu vilianzishwa Lilongwe mwaka wa 1965 baada ya kazi kugawanywa na ile ya Zimbabwe. Katika mwaka wa 1971 Jumuiya ya Wabatisti wa Malawi iliundwa.

Watu wa Malawi ni wepesi sana wa kupokea injili. Kwa hivyo makanisa yameanzishwa huko kwa haraka sana. Mwisho wa mwaka wa 1980 kulikuwa na washiriki wapatao 57,634 katika nchi ya Malawi ambao ni wa makanisa ya Kibatisti.

Sehemu ya Pili: Wabatisti Katika Zambia

Vikundi vingi vya Wabatisti vimekwisha fanya kazi katika nchi ya Zambia. Wabatisti wa kutoka Ulaya waliyaanzisha makanisa kati ya Wazungu wahamiaji wakulia. Katika mwaka wa 1905 wamisheni wawili walienda mpaka Zambia (ilijulikana kama Northern Rhodesia) kutoka Nyasaland Industrial Mission. Walienda kwenye sehemu za kuchimba madini ya shaba na kuanzisha kazi yao kati ya Walumba. Katika mwaka wa 1913 waliomba msaada kutoka kwa Wabatisti wa Afrika Kusini. Pia wamisheni kutoka nchi za Scandinavia walikaribishwa kuja kusaidia. Walianzisha kazi kati ya Walumba katika mwaka wa 1831. Wamisheni hao waliendelea na kazi ya kushuhudia.

Southern Baptist Convention ya Amerika, kwanza iliwatuma wamisheni Zambia (mbeleni Northern Rhodesia) katika mwaka wa 1959. Mwaka ule Tom na Mary Small na Zeb na Evelyn Moss waliondoka Zimbabwe na kwenda mpaka Kitwe. Ted na Verna Savage walijiunga nao katika mwaka wa 1960 wakafungua kazi ya Mfulira katika sehemu za kuchimba madini ya shaba.

Jumba la uchapishaji lilianzishwa mwaka wa 1961 katika mahali panapoitwa Broken Hill. Baadaye lilihamishwa na kupelekwa Lusaka. Maelfu ya watu wamekwisha kuwa Wakristo kwa sababu ya kazi inayofanywa na Bible Way Correspondence School (yaani, shule ya kujifunza Biblia kwa njia ya Posta). Redio pia imesaidia sana kutangaza injili kwa watu wengi wanaokaa Zambia. Kampuni ya Zambia ya utangazaji imetenga wakati mwingi sana kwa vipindi vya mahubiri ya Kibatisti. Seminari ilifunguliwa Zambia katika mwaka wa 1967.

Katika mwaka wa 1964, Zambia ilipata uhuru wake chini ya uongozi wa Kenneth Kaunda. Nayo Jumuiya ya Wabatisti wa Zambia ikaanzishwa mwaka huo. Karibu mwisho wa mwaka wa 1980 makanisa ya Kibatisti ya Zambia yalikuwa na washiriki wapatao 8,124.

Sehemu ya Tatu: Mwanzo wa Kazi Katika Zimbabwe

Kwanza Wabatisti waliingia katika Zimbabwe wakiwa wakaaji. Waliomba wasaidiwe katika mahitaji yao ya kiroho. Wazungu wakulima waliomba msaada kutoka kwa Wabatisti wa Afrika Kusini. Mchungaji kutoka Afrika Kusini alifika katika mwaka wa 1920. Alianza kuwahudumu Wabatisti waliokuwa katika Gwelo, Bulawayo, Salisbury, Ursapi na Umtali mpaka mwaka wa 1925. Naye Joshua Monama alijiunga kufanya kazi pamoja naye mpaka mwaka wa 1928. Kanisa liliundwa katika mwaka wa 1928 na likajiunga na Baptist Union of South Afrika.

Hata hivyo kule katika nchi ya Uhindi watu wa kule huwafuga ndovu ili waweze kufanya kazi. Ndovu wa kule huchukua mizigo. Hukokota na husukuma mizigo mizito. Ndovu wa bara Hindi ni wadogo kushinda ndovu wa bara Afrika. Hata hivyo ni wanyama wakubwa na ni wenye nguvu sana. Kwa nini ndovu wa hapa huwa waharibifu hivi, lakini ndovu wa nchi nyingine huwa msaada mkuu katika kufanya kazi? Sababu ni kwamba mmoja ametawaliwa, lakini mwingine bado hajafundishwa.

Kuwa mpole ndio kuwa na kiasi. Ni mtu kujitawala. Kuliko kusema upesi kwa sauti kuu na kwa hasira, mtu mpole hutawala hasira yake. Yeye hujitawala na kutambua haki za watu wengine kuliko kujifanya kila mara kuwa mbele na wa kwanza katika kupata vitu.

Kuwa mpole siyo kuwa mnyonge na kuwafanya watu wengine wamkanyage au kumfanya kuwa duni. Yeye si mwoga. Ana nguvu, bali ni mwenye fadhili. Mtu mpole atasimama imara katika mambo yaliyo haki. Maisha yake hutawaliwa na Mungu, wala siyo tamaa zake mwenyewe.

Wale walio wapole wameahidiwa kwamba watairithi nchi. Wale walioingia katika nchi ya Ahadi ni wale tu waliomtumainia Mungu. Wenyeji waliingia nchi hiyo ili wawe na amani, na Mungu aliwapa nguvu za kuwashinda. Siku hizi Mungu amewaahidi Wakristo kuwapa maisha mapya. Kwa maisha haya mapya Mkristo aliye mpole anaweza kuishi hapa duniani akiwa na *amani* kati yake na watu wale wengine. Mungu anampa *nguvu* za kushinda shida kwa sababu ametawaliwa na Mungu.

Sehemu ya Pili: Furaha kwa Ajili ya Rehema

"Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema" (Mathayo 5:7). Yesu alisimulia habari za mtumwa mmoja aliyewiwa na bwanaye deni kubwa. Mwenye mtumwa huyo

SEPTEMBER

Mpango wa Pili

FURAHA KATIKA KUISHI MAISHA YA KIKRISTO**Kiini cha Mwezi:** Furaha ya Kweli**Maandiko ya Ibada Fupi:** 1 Petro 2:1-3**Kifungu cha Kukumbuka:***"Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema."**Mathayo 5:7***Utangulizi:**

Maisha ya Kikristo ni maisha yenye furaha. Basi kwa nini Wakristo wengine hawaonekani kuwa wenye furaha? Pengine hawajakomaa katika imani yao. Ikiwa Mkristo amezaliwa, ni lazima akue. "Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoishiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu" (1 Petro 2:2).

Mtu huwa amezaliwa upya ikiwa amemwamini Yesu. Sasa amekwisha okoka, yeye ni Mkristo, lakini ni lazima akue ikiwa atakuwa kama Yesu. Mkristo yule ambaye hakui hana furaha. Mkristo hukua kwa kujaribu kuyafanya maisha yake kuwa kama maisha ya Yesu. Leo tutajifunza juu ya furaha katika kuishi maisha ya Kikristo.

Sehemu ya Kwanza: Furaha ya Kutawala Maisha Yake

Demasi
"Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi" (Mathayo 5:5). Mpole ni mtu wa aina gani? Je, ni mtu mnyonge? Je, ni mtu yule ambaye hakasiriki? Biblia inasema kwamba Yesu alikuwa mpole lakini hakuwa mnyongel! Na hata siku moja alikasirika sana alipowafukuza wenye kubadilisha pesa hekaluni.

Je, umemwona ndovu aliyekasirika? Hulia mlio wa tarumbeta na huenda kwa mwendo wa kishindo. Hukanyaga mimea na huvunja miti. Mharibifu hivi! Ana nguvu jinsi ganil

Nayo makanisa mengine yaliweza kuanzishwa katika miji kuliko kuwa na Wazungu. Katika mwaka wa 1948 Rhodesia Baptist Association iliundwa ikiwa na wajumbe kutoka kwa makanisa matano.

Wafrika wengi kutoka Malawi waliokuwa Wabatisti walifika kufanya kazi katika mashamba ya Wazungu katika nchi ya Zimbabwe. Naye Daniel Malekebu aliyekuwa kiongozi wa Providence Industrial Mission katika Malawi alitembelea Zimbabwe katika mwaka wa 1934 ili akutane na Wabatisti wale waliokuwa katika mashamba hayo. Aliendelea kufanya hivyo kwa muda wa miaka mingi na waliweza kupata washiriki wengi.

Sehemu ya Nne: Wabatisti Katika Zimbabwe

Hakukuwa na kazi nyingi ya Kibatisti kati ya Wafrika wa Rhodesia mpaka Clyde na Hattie Dotson, Wabatisti kutoka Amerika walipofika na kuanza kufanya kazi huko katika mwaka wa 1930. Waliwaomba Southern Baptist Convention kuwatuma huko lakini pesa hazikuweco. Kwa hivyo, Dotson na jamaa yake walishuhudia huko kwa muda wa miaka ishirini wakitegemezwa na Wazungu wengine wa Zimbabwe na makanisa fulani ya Amerika. Mnamo mwaka wa 1950, Southern Baptist Convention ilianza kuwatuma wamisheni Rhodesia. Bwana Dotson na mkewe ndio waliokuwa wamisheni wa kwanza kuchaguliwa na Southern Baptist. Ralph na Betty Bowlin pia walichaguliwa na wakaenda Gatooma. Kanisa lilianzishwa huko katika mwaka wa 1950.

Wabatisti walipewa ardhi katika Zimbabwe katika sehemu inayopakana na Sanyati ambayo ni mbuga za kuhifadhi wanyama. Zamani hizo hakukuweco shule vijijini, kwa hiyo Wabatisti walianzisha shule. Hakukuwa na msaada wa wote wa utabibu kwa watu waliokaa vijijini. Wabatisti walifungua hospitali huko mwaka wa 1953. Daktari Giles Fort na mkewe,

Wana Ann, ambaye pia alikuwa daktari, walifanya kazi pamoja na mwiuguzi aliyeitwa Monda Marler.

Wabatisti walifungua Seminari kule Gwelo, katika mwaka wa 1955. Jumba la Uchapishaji lilijengwa katika Bulawayo katika mwaka wa 1961. Kazi ya uchapishaji ilikuwa imesimamiwa na wamisheni Logan na Virginia Atnip. Duka la kuuza vitabu lilianzishwa mwaka wa 1963 na kazi ya Redio na Televisheni katika mwaka wa 1968.

Katika mwaka wa 1963 Jumuiya ya Wabatisti wa Afrika ya Kati iliundwa. Wakati mmoja Zimbabwe, Zambia, na Malawi, zilikuwa na mwungano uliojulikana kama "Federation of Central Africa". Wabatisti walikuwa wamepanga kueneza ushuhuda wao katika sehemu zote za mwungano huo. Katika mwaka wa 1963, mwungano huo ulivunjika na kazi ya Wabatisti katika nchi hizo ikagawanyika. Halafu Jumuiya yao ikaitwa "Baptist Convention of Rhodesia".

Baada ya miaka mingi yenye shida za vita, serikali mpya iliundwa katika mwaka wa 1980 chini ya Robert Mugabe, na kila mwananchi akiwa na haki ya kupiga kura. Nayo Jumuiya ya nchi hiyo ikachukua jina mpya la "Baptist Convention of Zimbabwe."

Katika mwisho wa mwaka wa 1980 katika nchi ya Zimbabwe kulikuwa na Wabatisti wapatao 12,851.

Mwisho:

Wabatisti wanazo kazi zaidi za kulipeleka jina la Yesu Kristo katika nchi zote za Afrika. Wengi wa babu zenu walifariki bila kusikia jina ya Yesu Kristo. Kungali kunao watu wengi ambao hawajamjua. Je, katika nchi yenu kunao watu ambao bado hawajamsikia? Je, kuna watu wanatamani mtu wa kuwaambia habari za Yesu? Je, wewe utawaambia? Hatuwezi kubadilisha yale yaliyopita, lakini kwa nguvu zake Mungu, tunaweza kubadilisha mambo. Unaweza kuzifanya "Njia Zake Zijulikane."

itakulazimu kula chakula hicho kwa sababu walikupikia. Utaendelea kukila. Wamezidi kukuletea chakula. Nawe unaendelea kukila. Mwishowe, umeshiba kabisa! Huwezi kula zaidi ya hapo. Lakini waliokukaribisha wakizidi kukuletea chakula kingine cha aina nyingi. Ni chakula kizuri zaidi kuliko cha kwanza! Lakini sasa huna njaa tena. Hata ingawa ni chakula kizuri hukitamani.

Yesu alisema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa" (Mathayo 5:6).

Haki ni kama chakula kizuri. Lakini watu wengine hawakitaki. Wamekwisha jaza maisha yao na mambo mengine hata hawaoni njaa ya haki. Wametoshaka na hawatamani haki yake Mungu. Wametoshaka. Hawataki kupokea kile ambacho Mungu huwapa.

Mtu mwenye njaa anaweza kutoa pesa zake za mwisho kununua chakula kidogo. Mtu mwenye kiu anaweza kutoa cho chote ili apate maji ya kunywa.

Yule kijana alikataa uzima wa milele. Alikuwa amejazwa na mambo mengine hata hakuona njaa na kiu ya kutamani maisha yale ambayo Yesu alitaka kumpa. Alikataa kuacha hata jambo moja alilofurahia. Hakuona njaa hata kidogo ya uzima wa milele.

Haki yetu haitatosheleza. "Matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi" (Isaya 64:6). Tunahitaji kuwa na haki yake Mungu ipatikanayo katika kumwamini Yesu, "Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21).

Ameahidi kuwajaza wale wanaotamani kuwa na haki hii. Watajazwa na "Matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo" (Wafilipi 1:11).

Sehemu ya Pili: Heri Wenye Huzuni *Phyllis*

Kule mbali unaweza kusikia ngoma na mlio wa maombolezo. Kelele hizo zinaendelea usiku kucha na hata keshoye. Pengine jambo litaendelea kwa muda wa juma nzima. Mtu fulani amefariki. Watu wanaomboleza. Je, watapata faraja? Je, mtu hupata faraja ya kweli kwa ajili ya kuomboleza kwa muda wa siku nyingi? Au mwishowe anajisikia kwamba amechoka tu?

Yesu alisema, "Heri wenye huzuni; maana watafarajika" (Mathayo 5:4). Maana yake kusema hivyo ni nini? Kunayo mawazo matatu hapa:

1. Luka amesema, "Heri ninyi mliao sasa, kwa sababu mtacheka" (Luka 6:21). Wakristo wanaweza kuyapata mateso sasa, lakini baadaye watapatiwa dhawabu yao.

2. Heri wale wanaohuzunika kwa sababu ya dhambi na mateso ya watu wengine katika ulimwengu. Wakati Yesu alipoyaona makutano ya watu, "Aliwahurumia." Yesu alikata shauri kuacha nyumbani kwake mbinguni aje hapa duniani ili ateswe kwa ajili ya wengine.

3. Heri wenye huzuni na kuvunjika moyo kwa sababu ya dhambi zao. Paulo alisema, "Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto" (2 Wakorintho 7:10). Toba hii hufungua mlango uleto msamaha wa dhambi na hufuatwa na faraja.

Wale wanaohuzunika na wengine au kwa sababu ya dhambi zao wanaahidiwa kwamba watafarajiwa.

Sehemu ya Tatu: Heri Wenye Njaa na Kiu *Jerita*

Pengine umekaribishwa katika nyumba ya rafiki yako. Kwa sababu wewe u mgeni wao, watakupikia chakula. Chakula kile wanachokuletea siyo chakula ukipendacho sana, lakini

AGOSTI

Mpango wa Kwanza

MABADILIKO NDANI YA MTU**Kiini cha Mwezi:** Ukristo Huyaleta Mabadiliko**Maandiko Matakatifu:** Waefeso 4:22-24**Kifungu cha Kukumbuka:**

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazamal yamekuwa mapya."

*2 Wakorintho 5:17***Kiongozi wa Mpango:**

Yesu alipokuja ulimwenguni, alimdhihirishia mwanadamu njia mpya ya maisha. Wayahudi walizoea kufuata torati za Musa alizowapa kutoka kwake Mungu. Hata alijitengenezea torati zingine walizojiongeza zaidi. Walizifuata torati hizi kwa muda wa miaka elfu nyingi.

Lakini Yesu alipokuja, aliwafundisha habari za mambo yale ambayo hawakuyafikiria. Aliwafunulia Mungu kwa njia mpya. Yesu alisema kwamba alikuja kuyafanya mafundisho ya Musa kuwa dhahiri (Mathayo 5:17). Watu walipoanza kusikiliza Yesu na kuyakubali mafundisho yake, walianza kuyafanya mambo kwa njia tofauti. Paulo aliandika akisema katika 2 Wakorintho 5:17, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazamal yamekuwa mapya."

Sehemu ya Kwanza: Je, Tunapata Kuwa Kiumbe Kipya Kwa Njia Ipi?

Tumezaliwa kwa miili fulani. Tutakuwa na miili hiyo mpaka tutakapokufa. Lakini je, mwili hukaa katika hali moja? La. Mtazame mtoto mchanga. Halafu mtazame mtoto aliye mkubwa kidogo. Kisha mtazame mvulana au msichana mwenye umri wa

miaka kumi na miwili. Mwishowe mtazame mtoto aliye mzima na amekomaa. Halafu mtazame mtu anayezeeka. Unaweza kuona vile mwili wa mwanadamu unavyobadilika katika maisha yake.

Ni vigumu kidogo kuyaona mabadiliko mengine, lakini tunajua ya kwamba yapo. Unaweza kuona mtoto anapoanza kutembea na kuongea. Tunajua ya kwamba mabadiliko yameanza kuonekana ndani yao. Bongo zao zinaanza kufikiria.

Pia, ndani ya mtu kuna nafsi. Hii ndiyo Paulo anayosema kwamba mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya. Mwili unabaki kuwa mwili, uleule, lakini kunayo mabadiliko katika nafsi yaani roho.

Sehemu ya Pili:

Je, ni kitu gani kinachokuwa ndani ya mtu kabla ya kumwamini Kristo? Katika Waefeso 4:22, Paulo ametuambia, "Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya." Yale ambayo yamo ndani ya mtu kabla ya kumkubali Kristo ni mambo ya kudanganya." Yale ambayo yamo ndani ya mtu kabla ya kumkubali Kristo ni mambo ya kudanganya, ni mambo maovu. Mambo hayo ndiyo yanayoleta dhambi. Hayo hututenganisha na Mungu kwa sababu Mungu ni mtakatifu.

Wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi katika bustani ya Edeni, walikubali kuongozwa na maovu yaliyokuwa ndani yao. Walichagua kumsikiliza Shetani kuliko kumtii Mungu. Kwa sababu ya jambo hili jamii ya wanadamu walitenganishwa na Mungu. Katika hali hiyo ya kutenganishwa, mwanadamu huutii utu wake wa kale. Hufanya mambo ya kusema uongo, kuiba, na huwadanganya wengine, hata hua. Hizo zote ni dalili za kuonyesha kwamba hamtii Mungu. Lakini tunapopata kuwa Wakristo mambo hayo yote huondolewa. Mambo hayo yote yalikuwa ya utu wa kale ambao tulikuwa nao bila Kristo.

Sehemu ya Kwanza: Heri Walio Maskini

Rosaline

"Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mathayo 5:3).

Watu wanahamia katika miji mikuu ya Afrika siku hizi. Watu huenda kuishi katika miji hata ikiwa hawana kazi wala pesa. Jel watu hao wanaishi wapi? Wao hukaa na watu wa ukoo wao mpaka watakapofukuzwa. Baada ya hayo wanajijengea vyumba vya karatasi na miti na karatasi za "plastic." Tena wanakata mabati ya debe kwa kutengeneza dari. Kila siku wanatafuta chakula cha kuwafanya waishi. Mara kwa mara chakula kama hicho hupatikana katika mapipa ya takataka. Wakati mwingine mama huwatumia watoto waende wakaombe vyakula. Nao wakati mwingine mama huuza mwili wake. Daima wanapigana na panya wanaotaka chakula chao. Siku fulani City Council hutuma tingatinga kwenda kuangusha nyumba zote zisizo halali. Baada ya kubomolewa watu hao huachwa bila mahali pa kulala. Watu hao ni maskini. Hawana kitu. Wanajua ya kwamba hawana kitu. Wao hawana la kufanya. Hawawezi kujisaidia wenyewe.

Yesu alisema, "Heri walio maskini wa roho." Je, maskini wa roho ni akina nani? Ni watu wale ambao hawana kitu cha thamani ndani ya roho zao na maisha yao. Wanajifahamu kwamba hawana kitu. Hawawezi kujisaidia wenyewe. Hawana njia wenyewe kupata msaada. Kile wawezacho kufanya ni kumgeukia Mungu awasaidie. Kwa sababu wanajua hawana kitu kusaidia na roho zao, ni lazima wamwamini Mungu kabisa ili awasaidie.

Mtu yule anayejitoa kabisa kwake Mungu ameahidiwa ufalme wa mbinguni. Yaani ni sawa na ufalme wa Mungu. Mtu yule anayemtegemea Mungu kabisa anamtumainia Mungu kuwa mfalme wake. Mungu ndiye mtawala wa maisha yake. Yesu ni mtawala wa ufalme wa mbinguni.

SEPTEMBER

Mpango wa Kwanza

FURAHA WAKATI WA HITAJI LETU KUU**Kiini cha Mwezi:** Furaha ya Kweli**Maandiko ya Ibada Fupi:** Zaburi 34:6**Kifungu cha Kukumbuka:***"Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao."**Mathayo 5:3***Utangulizi:**

Je, ni kifungu gani unachopenda sana katika Biblia? Pengine ni hotuba ya Yesu mlimani (Furaha ya kweli). Watu wengi huvipenda vifungu hivi vinavyopatikana katika Mathayo 5:1-12. Vifungu hivi hueleza kiini cha umuhimu wa imani ya Kikristo. Yesu alitaka wafuasi wake wayasikilize mafundisho yake. Aliwaita pamoja. Kisha akaketi na kuanza kuwafundisha. Zamani zile waalimu walikuwa wakiketi chini ikiwa walikuwa na jambo muhimu la kufundisha.

Pengine watu walishangazwa sana na maneno ya Yesu. Matamshi yake yalikuwa kinyume cha mambo yale ambayo ulimwengu hufikiria kwamba ni ya kweli. Matamshi haya yanaeleza furaha tele ya Mkristo *duniani*.

Matamshi hayo yanaweza kugawanywa katika sehemu tatu. Leo tutajifunza juu ya furaha za Mkristo anapoupata msaada kwa shida za maisha: Umaskini, njaa, huzuni. Juma lijalo tutajifunza juu ya furaha inayopatikana katika kuishi maisha ya Kikristo katika upole, rehema, katika maisha ya utakatifu na amani. Juma la kufuata tutajifunza juu ya furaha ipatikanayo kwa kuteswa kwa ajili ya Yesu Kristo.

Sehemu ya Tatu:

Kuwa kiumbe kipya ni kusema nini? Paulo amesema, "Mkavae utu mpya, uliombwa kwa namna ya Mungu katika haki ya utakatifu wa kweli" (Waefeso 4:24). Utu upya hufanywa, ukifanana na Mungu. Je, Mungu alisema nini alipokata shauri kumwamba mwanadamu? Alisema, "Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu" (Mwanzo 1:26a). Tunatakiwa tuwe kama Mungu. Lakini kwa sababu ya dhambi, tulipoteza hali hii ya kufanana naye. Sasa tunapomwamini Kristo kama Mwokozi na kumpokea kama Mwana wa Mungu, tunaauvaa tena utu wa kufanana na Mungu.

Je, kutakuwa vipi tukifanana na Mungu? Tutakuwa watakatifu kama vile Mungu alivyo mtakatifu. Tutakuwa wenye haki mbele zake Mungu. Mungu anapotutazama, hataona utu wetu wa kale, wenye dhambi na uovu. Ataona utakatifu wetu kwa sababu tumefichwa ndani yake Kristo (Wakolosai 3:3). Kristo huzifunika dhambi zetu kwa damu yake iliyotolewa msalabani.

Tena tutakuwa watakatifu. Mungu alisema, "Basi mtakuwa watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (Walawi 11:45). Hatuwezi kuwa watakatifu ikiwa tutaendelea kuuweka utu wetu wa kale, kwa maana ni wenye uovu. Tutautwaa utu wetu ulio mpya, watu wengine wanaweza kuuona mfano wa Mungu ndani yetu.

Sehemu ya Nne:

Pengine umekwisha kumjua mtu fulani ambaye hakuwa Mkristo, lakini baadaye alipata kumwamini Kristo. Pengine hawezi kueleza yale yaliyopata kutukia katika maisha yake, lakini anajua kwamba amekwisha badilika. Anaweza kuwaambia wengine, "Mungu amenibadilisha". Kama yule

kipofu aliyeponywa na Yesu, anaweza kusema, "Mimi nalikuwa kipofu na sasa naona" (Yohana 9:25b).

Tukidumu katika utu wa kale wenye dhambi, wakati huo sisi huwa kama vipofu. Hatuwezi kuviona vitu vya kiroho na hata hatuwezi kuona vitu vya Mungu. Tunapompokea Kristo kama Mwokozi ndipo tunapovaa utu mpya. Ndipo tunapoanza kuviona vitu vya Mungu na kutembea katika njia zake.

Baada ya kuvaa utu mpya, ndipo watu wengine wanapoona mabadiliko ndani yetu. Watajua ya kwamba tumekwisha badilika. Wanaweza kuuona mfano wa Mungu ndani yetu.

Kiongozi:

Mtu anapomwamini Kristo na kumpokea kama Mwokozi wake, hatapenda kuendelea kutamani kutenda dhambi. Wakati mwingine anaweza kuwa mnyonge na kuanguka dhambini, lakini atajua ya kwamba ni kosa. Hata Paulo alisema ya kwamba aliendelea kupigana na hali ya maovu. Utu wetu wa kale hupenda kurudia ili ndipo ututawale. Hatupaswi kukubali jambo hili litukie.

Kwa sababu sisi tu watoto wa Mungu tunapata nguvu zake Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Nguvu hizi zinaweza kushinda nguvu za Shetani. Shetani ndiye huutawala utu wa kale.

Sasa tunao utu mpya, unaotawaliwa na Kristo. Tunaweza kuwa na utu kufanana na Mungu.

Maombi:

Tuombe kwamba tutamkubalia Kristo ayatawale maisha yetu ili tufanane na Mungu.

Madokezo ya Maombi:

Ebu na tuombe ili Mungu atuonyeshe jinsi ya kumfanya kuwa wa kwanza katika maisha yetu. Omba kwamba tutambue ni mambo yapi yanapaswa kuwa ya maana kwa Mkristo.

Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:19). Petro alifahamu kwamba siku ya hukumu atatoa habari mbele zake Mungu wala siyo mbele ya wanadamu. Jambo hili lilikuwa la maana sana katika maisha yake.

Sehemu ya Nne:

*Ukristo Huleta mabadiliko
shitani yeye kutachukua nafasi yake
2. Ikiwa sasa watu wote lakini 57 Kerosel*

Watu wengi wametoshaka kuishi maisha yao ya kale. Hawataki kuyaona mabadiliko. Ni vyepesi kuendelea kama vile wamezoea kutenda kuliko kukua au kubadilika. Katika Waefeso 4:15 Paulo alisema, "Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo."

Kama vile miili yetu haibaki katika hali ya kitoto, vivyo hivyo, mawazo yetu na roho zetu hazipaswi kubaki katika hali ya utoto wa maisha ya Kikristo. Ni lazima tujifunze mengi kuhusu mapenzi yake Mungu. Ni lazima tujifunze jinsi ya kufanana na Kristo. Ni lazima tujifunze kumkubali Roho Mtakatifu atuongoze.

Njia moja ya kukua ni hiyo ya kusoma Biblia, ambayo ni Neno la Mungu. Inatueleza jinsi tuwezavyo kuishi maisha ya Kikristo. Wanaume na wanawake wengi ambao hawakupata nafasi ya kuingia shuleni walipokuwa watoto wachanga wamekwisha ingia shule za watu wazima, au wamempata mtu ambaye ametoa wakati wake kuwafundisha kusoma. Walitamani sana kujua kujisomea Neno la Mungu wao wenyewe ili waweze kukua kwa njia zote ndani ya Kristo.

Kiongozi wa Mpango:

Kuupata ujuzi wa Neno la Mungu ni jambo la maana sana katika maisha ya Mkristo. Ebu sote na tujaribu kukua katika kumjua Kristo ili tuweze kuwasaidia wengine kukua pia. Ikiwa unajua kusoma, msaidie mtu mwingine kujifunza kusoma. Ikiwa hujui kusoma, jaribu kuitafuta shule au mtu mwingine awezaye kukufundisha.

AGOSTI

Mpango wa Pili

MAMBO YALE YANAYOTOWEKA

Kiini cha Mwezi: Ukristo Huleta Mabadiliko

Maandiko Matakatifu: Wakolosai 3:1-10

Kifungu cha Kukumbuka:

"Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu."

Wakolosai 3:3

Kiongozi wa Mpango:

Mtu anapofariki dunia, roho yake huacha mwili. Mwili wake hufichwa au huzikwa. Hauonekani tena. Paulo aliwaambia Wakolosai kwamba, ikiwa wamempokea Kristo kama Mwokozi, basi, wamekwisha kufa. Maana yake, wamekufa katika kuishi maisha ya kale, yaani, maisha ya dhambi. Sasa hawawezi tena kuwa watumwa wa dhambi.

Alisema kwamba, sasa maisha yamefichwa pamoja na Kristo. Ikiwa jambo limezikwa, haliwezi kuonekana tena. Maisha ya Mkristo yamefichwa pamoja na Kristo. Utu wa kale hauwezi kuonekana. Kristo hufunika au huficha maisha yake ya kale na maisha yake. Wakati Mungu anapotutazama sisi kama Wakristo hawezi kuziona dhambi zetu. Huwa umefunikwa au kufichwa na damu yake Kristo.

Tunapokuwa Wakristo maisha ya dhambi hutoweka kutoka katika maisha yetu. Hayawezi kuonekana tena. Leo tutaongea juu ya mambo fulani ambayo tumekwisha kuyaacha.

Sehemu ya Kwanza:

Paulo aliwaambia watu wa Kolosai kwamba wavue mambo ya ulimwengu. (Usome Wakolosai 3:5-9). Kwanza, aliwaambia wayaondoe mambo ya zinaa. Hii inaweza kuwa aina yo yote ya

dhambi, jambo lo lote ambalo ni kinyume cha adabu njema. Mara kwa mara inafikiriwa kama dhambi ya kujuana kimwili. Pia Paulo ametaja dhambi ambazo ni za kufikiria na kuwaza. Tamaa za kutenda maovu ni dhambi na ni lazima iachiliwe mbali.

Uchoyo ni dhambi na ni lazima isulibiwe. Hii inaweza kuwa na hali ya kuabudu mali au kupenda kuwa na mamlaka kuliko kumwabudu Mungu. Mambo hayo huwa kama miungu ndani ya mawazo yetu.

Katika Injili ya Luka 19:1-10 tunaweza kusoma habari za Zakayo. Alikuwa mkuu wa watoza ushuru. Zamani zile watoza ushuru waliweza kuwatoza watu ushuru mwingi zaidi kuliko vile serikali ilivyoamuru. Walipata kuwa matajiri sana kwa sababu ya kuwalazimisha watu kulipa pesa nyingi. Alikubali tamaa yake ya kutaka utajiri iwe kama miungu wake.

Siku moja Yesu alipitia katika mji wa Yeriko mahali ambapo Zakayo aliishi. Yesu aliingia katika nyumba ya Zakayo na akala pamoja naye. Zakayo aliweza kufahamu kwamba alitenda dhambi. Alikubali kwamba maisha yake yalikuwa maovu. Alisema kwamba nusu ya mali zake atawapa maskini na kulipa mara nne zaidi ikiwa alimdanganya mtu katika kupata hizo mali. Yesu aliona kwamba Zakayo amekwisha badilika. Alisema "Leo wokovu umefika nyumbani humu." Utu wa kale uliondoka kutoka kwake Zakayo.

Sehemu ya Pili:

Mambo mengine ambayo Wakolosai waliambiwa waepukane nayo ni hasira, ghadhabu, maovu, matukano, matusi na kuambiana uongo (Wakolosai 3:7-10). Mambo hayo yote Paulo alisema, yalikuwa sehemu ya utu wa kale. Lakini sasa utu mpya haupatani na utu wa kale. Sisi Wakristo ni lazima tuyaache mambo hayo.

lilikuwa jambo la maana kuonekana na kutambulikana kwamba wao ni watu wa dini.

Yesu hakusema kwamba ni kosa kufunga na kuwapa maskini mali au kuomba mbele ya watu. Lakini alisema kuwa ikiwa tunafanya hivyo ili watu wapate kutuona hatutapata dhawabu kutoka kwa Mungu Baba. Kile kitu ambacho tutapata ni sifa kutoka kwa watu tu wanaotuna.

Tunapokuwa Wakristo, ni jambo la maana sana kufikiria vile Mungu anavyotuna kuliko vile watu wanavyotufikiria. Tutawatumikia, siyo kwa sababu ya sifa zao, lakini kwa sababu tunataka kumtumikia Bwana. Tutashiriki kile tulicho nacho pamoja na wengine, siyo kwa sababu tunataka kusifiwa na wao, lakini kwa sababu tunataka Mungu apewe sifa.

Sehemu ya Tatu:

Jambo la maana sana katika maisha ya Wakristo ni kumsifu Mungu, wala siyo watu. Wakati Yesu alipowalisha mkate watu wapatao elfu tano, walitaka kumfanya mfalme. Walifikiria kwamba kila mara atawalisha kwa chakula na hawataona njaa tena. Yesu aliweza kuwa mtawala wao, lakini alijua kuwa hiyo siyo mapenzi yake Mungu. Kusudi la Mungu lilikuwa kumtuma Yesu hapa duniani awe Mwokozi wa watu wote, wala sio mtawala wa watu wa zamani hizo. Yesu alifahamu kwamba ni lazima ayafanye mapenzi ya Mungu. Baada ya Yesu kusulubiwa msalabani na kuzikwa na kufufuka, alipaa kwenda mbinguni. Petro pamoja na mitume wale wengine aliwahubiria watu wengi katika Yerusalemu. Viongozi wa dini wa Kiyahudi waliwashika na kuwaamuru kwamba wasihubiri tena habari za Yesu.

Lakini waliendelea kufanya hivyo. Baadaye mitume waliiletwa mbele ya viongozi hao. Waliwashitaki kwamba walikataa kutii amri zao. Petro alisema, "Imetupasa kumtii

mtu huyo alienda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Mtu huyo alitaka uzima wa milele. Alikuwa mtu mzuri, yaani, alishika amri. Hata hivyo alifahamu ya kwamba jambo hilo halitoshi, alitaka kutenda mengi zaidi. Aliposikia majibu ya Yesu, alifikiraje? Tamaa yake ya kuupata uzima wa milele haikuwa na nguvu kama tamaa yake ya kushika mali alizokuwa nazo na hata kutamani mali zingine zaidi. Hakutaka kuacha vitu vyote kama mali zake ili ndipo amfuate Yesu.

Katika masomo mengine yaliyopita tumeongea habari za kuuvua utu wa kale na kuuvaa utu upya. Maisha yetu mapya katika Kristo yanapaswa kuwa ni maisha ya kutoa kuliko kujipatia sisi wenyewe. Katika Waefeso 2:8-10, Paulo amesema kuwa tumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani kwa sababu ni kipawa chake Mungu. Wokovu wetu hautokani na vitu vile ambavyo sisi wenyewe tumekwishatenda, lakini ni kwa njia ya kazi ya Yesu Kristo. Hatuwezi kuupokea wokovu kwa njia ya kazi njema, kama vile yule kijana tajiri alivyotaka kufanya. Hata hivyo, baada ya kuokolewa kwetu, kusudi letu linapaswa kuwa kutenda kazi njema ambayo Mungu amekwisha tayarisha kwa ajili yetu. (Waulize wanawake kutaja kazi njema ambazo Wakristo wanapaswa kuzifanya.)

Sehemu ya Pili:

Tunaweza kusoma kutoka katika Mathayo sura ya sita vile Yesu alivyosema kuhusu Mafarisayo. Dini yao ilikuwa ya maana kwao. Walitaka kila mtu ajue kwamba wao walikuwa watu wa dini sana. Walipofunga kula chakula, walionekana wenye huzuni na wenye njaa ili kila mtu apate kuona kwamba wamefunga na wafikiriwe kuwa wao ni wema na ni watu wa dini. Mara kwa mara walipowapa maskini kitu, walisema tarumbeta ipigwe ili waonekane na watu wote. Waliomba nje ili waonekane wao ndio wanaomba sana. Walifikiria kuwa

Mambo kama hasira, chuki na kusema uongo ni mambo yanayoharibu kutembea kwetu pamoja na Bwana. Yanapinga kukua kwetu kiroho. Pia mambo hayo hutuzuia kutowashuhudia wale waliopotea wanaotuzunguka. Watu wanafikiria kwamba Wakristo ni watu wenye upendo na utimilifu. Kweli, hivyo ndivyo inavyostahili kuwa. Watu ambao hawajaokoka wakiona kwamba tunakasirika, tunawachukia watu wengine na kusema uongo, wanawezaje kuamini kwamba sisi tu Wakristo?

Hadithi inasimuliwa kuhusu mtu mmoja aliyemchukia mtu mwingine. Yule mtu aliyesingiziwa alipoteza kazi na marafiki zake. Aliishi maisha yasiyo na furaha. Siku moja, mwenye kusema uongo alizitubu dhambi zake. Aliuliza, "Nawezaje kutengeneza kosa hili?" Aliambiwa ajaze manyoya ya kuku ndani ya gunia. Alifanya hivyo na akarudi. Akaambiwa, "Sasa, fungua gunia. Kisha mwaga hayo manyoya." Alitii agizo hili. Halafu aliambiwa, "Sasa, enenda uokote manyoya hayo yote."

"Siwezi," alijibu. "Upepo umewatawanya hayo yote." "Hivyo ndivyo ilivyo kuhusu kwa kusema uongo," akijibiwa. "Baada ya kuyatamka, huwezi kuyarudisha."

Hadithi, hii inaweza kutusaidia kuona kwamba ikiwa sisi Wakristo tutaendelea kutenda dhambi, ushuhuda wetu utapotea kama vile manyoya yalivyopotea. Ni lazima tuachane na dhambi zetu. Zinapaswa kutoweka kutoka katika maisha yetu.

Sehemu ya Tatu:

Pengine tuna desturi katika maisha yetu ambazo tunapaswa kuziacha kabla ya kuwa Mkristo. Tulikuwa tukitumainia vitu kuliko kumtumainia Mungu. Wakati Mungu alikuwa akizitoa torati kwa Waisraeli, aliwaambia wasifuate desturi za watu waliokuwa wakiishi katika nchi ile ambayo alitaka kuwapa. Watu hao walikuwa wakiwategemea wachawi.

Walitegemea hirizi ili ziwaponye au ndipo ziwalinde. Lakini Mungu aliwaambia Waisraeli wasifanye mambo hayo.

Watu wasiyo Wakristo waliwaona watu wanaojiita Wakristo wakitumia hizo hirizi, hawawezi kuamini kwamba watu hao ni Wakristo wa kweli. Wanaona kwamba wangali wakiamini uchawi wala siyo Mungu.

Hapo kale mwanamke mmoja kijana alikuwa na ugonjwa uliomfanya apoteze ufahamu kwa sababu ya kutoka damu. Wachawi walimpa hirizi, lakini hazikumsaidia. Alikata shauri kwamba ataanza kuhudhuria makanisa kadha wa kadha, lakini hakusaidiwa. Mwishowe, mchungaji wa kanisa la Kibatisti alimwambia kwamba ni lazima amwamini Yesu kisha aziweka shida hizo mikononi mwake Mungu. Siku moja baada ya kumkubali Kristo, alipotewa na ufahamu wake tena. Alipoamka, jamaa zake walikuwa wakijaribu kumweka hizo hirizi. Alikataa kuyafuata mawazo hayo. Alisema kwamba amekwisha mkubali Yesu Kristo na aliziacha njia za kale. Mwishowe alipata msaada wa kuponywa ugonjwa wake.

Kiongozi wa Mpango:

Tunapoendelea kujifunza Biblia, tunaweza kuyaona mambo mengi ambayo tumeambiwa tuyaondoe kutoka katika maisha yetu. Ikiwa tutaendelea kuishi katika utu wa kale, huwa hatumwamini Kristo kwa kweli.

Madokezo ya Maombi:

Tumwombe Mungu kwamba atatusaidia kuondoa kutoka katika maisha yetu mambo yale yanayotuzuia kumtegemea Kristo.

AGOSTI

Mpango wa Nne

MAMBO MAPYA MUHIMU

Kiini cha Mwezi: Ukristo Huleta Mabadiliko

Maandiko Matakatifu: Mathayo 19:16-26

Kifungu cha Kukumbuka:

"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa Yeye."

Wakolosai 3:17

Kiongozi wa Mpango:

Ni jambo lipi muhimu katika maisha yako? Kwa watu wengine elimu ni kitu cha maana sana. Kwa watu wengine, pesa ni kitu cha kwanza kilicho muhimu. Nao watu wengine wanapenda uongozi. Wanataka kuwatawala watu wale wengine. Je, mambo hayo yanayo maana gani? Ikiwa mambo hayo ni ya maana kwako kuliko kitu kingine cho chote, sikiliza vile Yesu alivyosema.

Sehemu ya Kwanza:

Katika hadithi ipatikanayo katika Mathayo 19:16-26, kijana mmoja alimwendea Yesu akamwuliza ni kitendo gani angetenda ili apate uzima wa milele. Naye alijibu akamwambia kwamba anapaswa kushika amri. Naye huyo kijana akauliza ni amri gani. Naye Yesu alimjibu kwa kuweka orodha ya amri ambazo zinaeleza uhusiano wetu na watu wengine, yaani, "Usiue," "Usizini," "Usiibe" na kadhalika. Naye alijibu, haya yote nimeyashika, nimepungukiwa na nini tena?

Yesu alimjibu akamwambia, "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo nifuata." Tunaambiwa kwamba

amemwombea kwa muda wa miaka mingi. Mwishowe jamaa zake walipata kuungana katika Kristo.

Kiongozi wa Mpango:

Tunapokuwa Wakristo, uhusiano wetu hubadilika. Watu wasio Wakristo wataonekana wakiwa katika kinyume cha maoni yetu. Hatutapenda kushirikiana katika kutenda mambo tuliyokuwa tukitenda nao hapo mbeleni. Tutakumbuka kuwaombea na kuwashuhudia, lakini hatutatenda dhambi pamoja nao.

Wakati mwingine watu hutenganishwa na jamaa zao wanapompokea Kristo. Ikiwa mtu amekubali kumpokea Kristo, mara kwa mara jamaa za mtu huyo humlazimisha kuondoka nyumbani. Lakini katika Mathayo 19:29 Yesu alisema kwamba yeyote aliyeacha nyumba na jamaa zake kwa ajili yake atapokea mara mia na kuurithi uzima wa milele.

Ni furaha jinsi gani, ikiwa kumpokea Kristo kutaleta jamaa na marafiki katika Kristo. Marafiki wapya tunaowapata ambao ni ndugu na dada katika Kristo hutufanya kuwa jamaa kubwa. Tunashiriki urithi wa uzima wa milele na utukufu wa Yesu Kristo mwenyewe.

Madokezo ya Maombi:

Tumshukuru Mungu kwa ajili ya ushirika tunaoshirikiana na Wakristo wenzetu pamoja na Kristo mwenyewe kwa sababu ya kifo chake msalabani. Tuwaombee jamaa na marafiki ambao hawajaokoka.

AGOSTI

Mpango wa Tatu

MABADILIKO KATI YA MTU NA MWENZAKE

Kiini cha Mwezi: Ukristo Huleta Mabadiliko

Maandiko Matakatifu: Mathayo 5:43-48

Kifungu cha Kukumbuka:

"Amri mpya nawapā, mpendane kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo."

Yohana 13:34

Kiongozi wa Mpango:

Zamani za Agano la Kale watu walipewa torati za kufuata. Zikiwa torati ngumu. Wale ambao wangethubutu kuzivunja wangedhibiwa vikali sana. Ilikuwa mtu akiiba kitu cha mtu mwingine au kumwumiza mwenzake, naye atafanyiwa hivyo.

Lakini Yesu alifundisha jambo lingine mpya. Alifundisha kwamba, Wakristo hawapaswi kujilipiza kisasi kwa adui zao, au wale waliowatendea makosa. Yesu aliwaambia wawapende adui zao na kuwatendea mema wale waliowaudhi. Maneno hayo yalibadilisha maisha ya Wakristo wapya. Kwa kuitii amri hii mpya ya Yesu, waliweza kueneza habari njema za pendo la Mungu ulimwenguni mwote.

Sehemu ya Kwanza:

Watu wanapenda kushirikiana pamoja na watu wanaoweza kupatana nao, na wanaopenda kufanya mambo yanayofanana. Kabla watu hawajapata kuwa Wakristo, hasa marafiki zao huwa sio Wakristo pia.

Kuwa Wakristo kunapaswa kuyabadilisha maisha yetu. Yesu aliwaamuru Wakristo kuwapenda watu wote. Tunaweza kuona tofauti zilizokuwa katika maisha ya Paulo. Kabla ya kukutana na Yesu, alikutumia wakati wake mwingi katika

kuwashika na kuwaweka gerezeni. Aliwachukia wale waliomfuata Kristo. Lakini baada ya kumpokea Kristo, alibadilika. Aliwapenda wale ambao hapo mbeleni aliwachukia. Hakuwapenda wafuasi wenzake Wakristo, bali aliwapenda pia maadui na alijaribu kuwaambia habari za pendo lake Yesu. Tunaweza kufuata mfano wake Yesu kuwapenda wenzetu hata kama ni maadui zetu.

Yesu alituachia kielelezo kizuri cha kufuata. Alikuwa ulimwenguni kufa kwa ajili ya wale waliokuwa wangali wenye dhambi (Warumi 5:8).

Sehemu ya Pili:

Yesu alisema kwamba watu wa dunia hii waliwachukia wafuasi wake pia. Mara kwa mara tunaona ya kwamba tunapokuwa wafuasi wake, tunawapoteza marafiki zetu wa zamani. Njia zetu haziwi njia zao tena. Wakati mwingine hata jamaa zetu ambao sio Wakristo wanatuchukia.

Mmisheni mmoja na mchungaji walienda kijiji kimoja kuhubiri Injili. Walikaribishwa na mtu mmoja wa kijiji hicho. Mtu huyu pamoja na baadhi ya jamaa yake walikuwa wamekwisha kumkubali Kristo. Lakini watu wengi wa kijiji chake walikataa. Lakini wakati ulifika ambao wale waliomkataa Kristo walikataa kwamba lbada isiendeleo katika kijiji chao. Siku moja mtu yule aliyemwamini Kristo alimtuma mkewe kurudi kijijini. Alipofika alikuta nyumba yao imeanguka na hakuna mtu aliyetaka kumpa yeye wala watoto wake mahali pa kulala. Waamini hao walilazimishwa kuondoka kijiji hicho na kuacha watu wa jamaa yao.

Yesu alisema, "Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili. Wala apendaye mwana au binti kuliko mimi hanistahili" (Mathayo 10:37). Ni lazima tutamani kuacha jamaa na marafiki zetu wa zamani kwa ajili ya Yesu.

Sehemu ya Tatu:

Hata ikiwa wengine wetu tutatenganishwa na jamaa zetu kwa sababu ya kumkubali Kristo, wengine wataona kwamba kumkubali Kristo kunaunganisha jamaa na marafiki pamoja.

Tunaposoma kitabu cha Filemoni katika Agano Jipya, tutaona hadithi ya mtumwa mmoja aliyetoroka kutoka kwa Bwana yake. Bwanaye aliitwa Filemoni, na alikuwa Mkristo. Alikuwa amekwisha kumkubali Kristo kwa sababu ya ushuhuda wa mtume Paulo. Mahali fulani mtumwa huyo alikutana na Paulo. Naye Paulo alimshuhudia huyo mtumwa Onesimo, na alimkubali Kristo kama Mwokozi wake. Paulo alimwandikia Filemoni barua na kumpelekea kwa mkono wa mtumwa Onesimo. Katika barua hii alimsihi Filemoni ampokee Onesimo tena katika nyumba yake, siyo kama mtumwa tu, bali zaidi kama ndugu Mkristo. Bwana na mtumwa wake walipatana tena kama ndugu katika Kristo.

Kulikuwa na mwanamke mmoja Mkristo aliyeolewa na mtu asiye Mkristo. Kwa muda wa miaka mingi huyo mwanamke alimwomba mumewe ili apate kuwa Mkristo. Mchungaji wa kanisa alienda kumshuhudia mtu huyu. Marafiki walijaribu kumshuhudia. Lakini kila mara alikataa kusikiliza. Kila mwaka kanisa lilikuwa na mikutano ya uamsho. Wakati fulani mtu huyo aliweza kuhudhuria mkutano, lakini hakuitikia mwito wa Bwana. Mwishowe, baada ya miaka kumi na mitano, mchungaji mpya aliitwa kuwa mchungaji wa kanisa. Alikutana na mtu huyu na alijaribu kuzungumza naye habari za Yesu, lakini mtu huyo hakisikiliza. Baada ya mwaka mmoja kupita, kanisa lilikuwa na mkutano mwingine. Wakati wa mkutano watu wengi waliokuwa wameombewa waliokoka. Usiku mmoja mtu huyo alihudhuria mkutano. Roho wa Mungu alizungumza naye na mwishowe alijibu mwito wake. Alimkubali Kristo kuwa Mwokozi wake. Mke wake alifurahi sana. Alikuwa